

**UCHANGANUZI MAKINIFU WA DISKOSI KATIKA VIKATUNI VYA
SHUJAAZ**

SAMMY LIANA DIMBU

**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Shule ya Mafuzu kwa Minajili ya Kutosheleza
Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha
Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA
NOVEMBA, 2021**

UNGAMO NA IDHINI

Ungamo la Mwanafunzi

Tasnifu hii ni kazi yangu na hajjawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa minajili ya kutosheleza shahada yoyote.

Sahihilipende..... Tarehe..... 09/11/2021

Sammy Liana Dimbu
AM12/29017/16

Idhini ya Wasimamizi

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Chuka.

Sahihilipende..... Tarehe..... 09/11/2021

Prof. John M. Kobia
Chuo Kikuu cha Chuka

Sahihilipende..... Tarehe..... 09/11/2021

Dkt. Allan Mugambi
Chuo Kikuu cha Chuka

HATIMILIKI

©2021

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhuswi kunakili, kuiga, kurudufisha, kuhifadhi kwa njia ya kielektroniki au kutoa vipengele fulani kwa namna yoyote ile bila idhini kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

TABARUKU

Kazi hii namtabarukia mwanangu Rylan Mwangale Liana na marehemu baba yangu
Christopher Dimbu Eliana.

SHUKRANI

Mafanikio ya utafiti huu yanahuisha wengi. Nitakosa fadhila iwapo sitawashukuru: Kwanza, namshukuru Maulana kwa kunijalia masomoni mwangu. Ninatoa shukrani kwa wasimamizi wangu Prof. John M. Kobia na Dkt. Allan Mugambi kwa ushauri wenu ambao umekuwa dira katika kukamilisha kazi hii. Ushauri ambao kila mara ulikuwa wa kunitia moyo.

Ninatoa shukrani kwa wahadhiri wangu wa kozi ya uzamili. Hawa ni pamoja na Prof. John M. Kobia, Dkt. Allan Mugambi, Bw. Kimathi Mwembu, Bw. Arthur Mutegi na Bw. Enock Matundura. Elimu niliyoipata kwao imenifaa katika kazi hii. Wanafunzi wenzangu Bi. Faith Mugo na Bw. Ken Mwangi shukrani za dhati kwa ushirikiano wenu katika kuwezesha midahalo mbalimbali ya kiusomi chuongi.

Shukrani kwa wote waliokosoa tasnifu hii. Kwa Mwalimu Mkuu, wa Shule ya Upili ya Ngurubani, Bw. Anthony Karwigi asante kwa ushirikiano wako nilipokuwa nikifanya kazi hii. Walimu wenzangu Bw. Michael Maina, Bi. Risper Njeri na Bw. David Gitau shukrani za kipekee kwa usaidizi wenu. Hatimaye, marehemu baba yangu, mke wangu Winrose Waihuini, mama yangu Phebe Kageha, dada yangu Liz Kavugwi na ndugu yangu Eric Lundu shukrani kwa kunihimiza kuendeleza masomo yangu. Kuna wengine ambao walifaa ingawa sijaweza kuwataja. Naomba radhi na kuwashukuru kwa dhati. Nawaombea nyote baraka kutoka kwa Mola.

IKISIRI

Vikatuni vina wajibu muhimu katika aushi ya watoto na vijana ulimwenguni. Huenda ndio sababu Karne ya 21 imeshuhudia ongezeko la tafiti kuhusu vikatuni. Utafiti huu ni Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi katika Vikatuni vya *Shujaaz*. Malengo ya utafiti yalikuwa: Kueleza namna muwala ulivyokuzwa katika vikatuni vya *Shujaaz*. Kufafanua mikakati ya mazoeaya kijamii katika vikatuni vya *Shujaaz* na kutathmini jinsi mahusiano ya uwezo yalivyowasilishwa katika vikatuni vya *Shujaaz*. Nadharia iliyongoza utafiti huu ni nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi. Maazimio ya nadharia hii ni kuwa matumizi ya lugha katika jamii huchukuliwa kuwa mchakato wa jamii. Lugha si zao la jamii tu bali ni nguvu muhimu katika kuunda michakato iliyochanya au hasi. Mojawapo ya madhumuni ya nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi ni kusaidia katika uchanganuzi wa diskosi ili kufichua imani za kiiikadi zinazochukuliwa kuwa za kweli na kukubaliwa katika jamii. Data ya utafiti huu ilitokana na sampuli ya nakala 35 zilizoteuliwa kimakusudi kwa kuzingatia uchanganuzi wa yaliyomo kwa mujibu wa maswali ya utafiti. Utafiti ulichukua muundo wa utafiti wa kmaelezo. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa njia ya udondoaji matini ilijojumuisha maandishi na michoro ya picha. Uchanganuzi wa data na matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo yaliashiria kuwa muwala hukuzwa na: mada, sauti za kionomatopeya, maandishi katika mandhari ya paneli, maelezo ya mwandishi na uzungumzi nafsi. Muwala uliokuzwa ni wa aina ya; mada, msuko na muwala wa kijumla. Unominishaji, jazanda, ujumlishaji, utata wa maana, deikisisi za nafsi ndio mikakati ya mazoea ya kijamii yaliyotumika kuwasilisha diskosi ya *Shujaaz*. Hatimaye, mahusiano ya uwezo yaliwasilishwa kuitia kwa wahusika, wahusika na vijana, wadhamini na vijana, hadhira na mtu mashuhuri na mahusiano ya uwezo baina ya uana. Utafiti huu unatoa mchango wa kiisimu kwa kufasiri lugha teule kama mkakati wa kuwashurutisha na kuwawekea vizingiti vijana ili kuwadhibiti. Pili, kufafanua mikakati iliyotumiwa na wenye uwezo ili kujitambulisha na vikundi maalumu katika jamii hasa vijana nchini Kenya. Utafiti huu unapendekeza kuwa tafiti za baadaye zifavye katika *Shujaaz* kwa kuzingatia masuala ibuka, majukumu ya sauti ya kionomatopeya kando na kukuza muwala na naratolojia.

ABSTRACT

Comic strips have played important role in the life of the children and youth in the world. Perhaps this is the reason the 21st Century has experienced a considerable increase in the study of comic strips. This research focused on the Critical Discourse Analysis of *Shujaaz* Comic Strips. The study was guided by the following objectives: To explain how coherence was achieved in *Shujaaz* comic strips. Elaborate discursive strategies used in *Shujaaz* comic strips and examine how power relations were manifested in *Shujaaz* comic strips. Critical Discourse Analysis theory was used in this study. The objective of this theory is to perceive language use as a social practice. Critical Discourse Analysis theory argues that language is not only a product of the community but also has the power to create social practices that are positive or negative. One aim of Critical Discourse Analysis theory in discourse analysis is to reveal the ideological beliefs that are perceived to be true. The data of this study was collected from a sample of 35 copies that were purposively sampled based on content analysis according to the research questions through words and picture drawings. The study used a descriptive design to collect and analyze the data. Findings indicate that coherence in *Shujaaz* discourse is achieved through the topic framework, onomatopoeic sounds, and the words in the panel, writer's description, and monologue. The types of coherence established were topic, both local and global coherence. Nominalizations, metaphors, generalization, ambiguity in meaning, and personal deixis were the discursive strategies used to present *Shujaaz* comic strips. In conclusion, the power relations were portrayed through: characters, characters, and the youth, the content sponsor(s) and the youth, the audience and prominent person(s), and gender power relations. This study contributes to existing linguistic knowledge by interpreting the selected language as a strategy deployed to regulate and reproduce the society to order and control the youth. Secondly, it can be used to elaborate strategies used by the elites to identify themselves with the special groups particularly the youth in Kenyan society. This research recommends further studies to be undertaken in *Shujaaz* comic strips with consideration on emerging issues, the function of onomatopoeic sound apart from enhancing coherence and narratology.

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI.....	ii
HATIMILIKI	iii
TABARUKU.....	iv
SHUKRANI.....	v
IKISIRI	vi
ABSTRACT.....	vii
YALIYOMO.....	viii
ORODHA YA VIELELEZO	xi

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI	1
1.1 Usuli wa Utafiti	1
1.2 Suala la Utafiti.....	6
1.3 Malengo ya Utafiti	6
1.4 Maswali ya Utafiti.....	6
1.5 Umuhimu wa Utafiti.....	7
1.6 Upeo wa Utafiti	7
1.7 Maelezo ya Istilahi	8
SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI	9
2.1 Dhana ya Vikatuni.....	9
2.2 Matumizi ya Lughya katika Vikatuni.....	11
2.3 Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi katika Matini.....	12
2.4 Misingi ya Nadharia	14
SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI	18
3.1 Muundo wa Utafiti	18
3.2 Uteuzi wa Sampuli	18
3.3 Utafiti wa Maktabani.....	19
3.4 Ukusanyaji wa Data	19
3.5 Uchanganuzi wa Data.....	19
3.6 Maadili ya Utafiti	20

SURA YA NNE: MUWALA KATIKA SHUJAAZ.....	21
4.1 Utangulizi	21
4.2 Mada na Muwala.....	21
4.3 Sauti za Kionomatopeya.....	26
4.4 Maandishi katika Mandhari ya Paneli	28
4.4.1 Wakati.....	28
4.4.2 Mahali	29
4.4.3 Hitimisho la Hadithi	31
4.4.4 Mabango ya Biashara	32
4.5 Maelezo ya Mwandishi.....	33
4.5.1 Wakati.....	33
4.5.2 Siku ya Kutokea kwa Tukio	36
4.5.3 Hitimisho la Hadithi	37
4.5.4 Usimulizi katika Nafsi ya Kwanza	38
4.6 Uzungumzi Nafsi.....	40
4.6.1 Uzungumzi Nafsi Uliowasilishwa kwa Michoro ya Picha	40
4.6.2 Uzungumzi Nafsi Unaowasilishwa kwa maandishi	42
4.7 Hitimisho.....	43
SURA YA TANO: MIKAKATI YA MAZOEA YA KIJAMII KATIKA SHUJAAZ	44
5.1 Utangulizi	44
5.2 Unominishaji	44
5.2.1 Hustla.....	44
5.2.2 Wazito.....	46
5.2.3 Fisi	47
5.2.4 Source	48
5.2.5 Magava	49
5.3 Jazanda	51
5.3.1 Wingu Jeusi	51
5.3.2 Kitu kilichoshikwa Mkononi cha Rangi Nyekundu	52
5.3.3 Mate Yanayodondoka.....	54
5.3.4 Michoro ya Vifungu vya Miraa	55
5.3.5 Bahari.....	56

5.4 Ujumlishaji	57
5.5 Utata wa Maana.....	58
5.5.1 Utata wa Kileksia.....	59
5.5.2 Utata wa Kimuundo	62
5.6 Deiksisi Nafsi	64
5.6.1 Deiksisi Nafsi ya Kwanza.....	64
5.6.2 Deiksisi Nafsi ya Pili	65
5.6.3 Deiksisi Nafsi ya Tatu	67
5.7 Hitimisho.....	68
SURA YA SITA: MAHUSIANO YA UWEZO KATIKA SHUJAAZ	69
6.1 Utangulizi	69
6.2 Wahusika.....	69
6.3 Wahusika Mashujaa na Vijana.....	72
6.4 Wadhamini na Vijana.....	74
6.5 Hadhira na Mtu Mashuhuri	76
6.6 Uana	78
6.6.1 Kubagua kwa Kujumuisha na Kutenga	79
6.6.2 Kubagua kupitia kwa Machukulio ya Kijamii.....	81
6.6.3 Ubaguzi kutokana na Vyeo.....	82
6.6.4 Kubagua kutokana na Uwasilishwaji katika Shughuli	84
6.7 Hitimisho.....	85
SURA YA SABA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	86
7.1 Muhtasari wa Utafiti.....	86
7.2 Hitimisho	87
7.3 Mapendekezo ya Utafiti wa baadaye	87
MAREJELEO	88
VIAMBATISHO	99
Kiambatisho 1: Orodha ya Ukaguzi	99
Kiambatisho 2: Kibali cha Utafiti kutoka kwa Chuo Kikuu cha Chuka	100
Kiambatisho 3: Kibali cha Utafiti	101

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo cha 1: Mada na Muwala.....	22
Kielelezo cha 2: Mada na Muwala.....	22
Kielelezo cha 3: Mada na Muwala.....	25
Kielelezo cha 4: Mada na Muwala.....	26
Kielelezo cha 5: Sauti ya Kionomatopeya	27
Kielelezo cha 6: Maandishi katika mandhari ya paneli	28
Kielelezo cha 7: Maandishi katika mandhari ya paneli	29
Kielelezo cha 8: Maandishi katika mandhari ya paneli	31
Kielelezo cha 9: Mabango ya Biashara.....	32
Kielelezo cha 10: Maelezo ya Mwandishi	34
Kielelezo cha 11: Maelezo ya Mwandishi	35
Kielelezo cha 12: Maelezo ya Mwandishi	36
Kielelezo cha 13: Maelezo ya Mwandishi	37
Kielelezo cha 14: Maelezo ya Mwandishi	38
Kielelezo cha 15: Uzungumzi nafsi	40
Kielelezo cha 16: Uzungumzi nafsi	42
Kielelezo cha 17: Unominishaji.....	45
Kielelezo cha 18: Unominishaji.....	46
Kielelezo cha 19: Unominishaji.....	47
Kielelezo cha 20: Unominishaji.....	48
Kielelezo cha 21: Unominishaji.....	49
Kielelezo cha 22: Jazanda.....	52
Kielelezo cha 23: Jazanda.....	53
Kielelezo cha 24: Jazanda.....	54
Kielelezo cha 25: Jazanda.....	55
Kielelezo cha 26: Jazanda.....	56
Kielelezo cha 27: Ujumlishaji.....	57
Kielelezo cha 28: Utata wa Maana	59
Kielelezo cha 29: Utata wa Maana	61
Kielelezo cha 30: Utata wa Maana	62
Kielelezo cha 31: Utata wa Maana	63
Kielelezo cha 32: Deiksisi Nafsi.....	64

Kielelezo cha 33: Deikisisi Nafsi.....	65
Kielelezo cha 34: Deikisisi Nafsi.....	66
Kielelezo cha 35: Deikisisi Nafsi.....	67
Kielelezo cha 36: wahusika	69
Kielelezo cha 37: Wahusika.....	71
Kielelezo cha 38: Wahusika.....	72
Kielelezo cha 39: Wahusika Mashujaa na Vijana.....	73
Kielelezo cha 40: Wadhamini na Vijana	75
Kielelezo cha 41: Hadhira na Mtu Mashuhuri.....	77
Kielelezo cha 42: Hadhira na Mtu Mashuhuri.....	78
Kielelezo cha 43: Uana	80
Kielelezo cha 44: Uana	81
Kielelezo cha 45: Uana	83
Kielelezo cha 46: Uana	84

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Utafiti

Diskosi ni lugha katika mchakato wa mawasiliano (Blommaert, 2005). Hivyo dhana ya diskosi ni lugha katika matumizi na hujikita katika mawasiliano na matendo ya washiriki ambayo huwekwa katika kategoria ya: kuwasiliana, kutagusana na majukumu ya kijamii kulingana na majukumu yao na hufungamanishwa na muktadha mahususi wa kijamii. Diskosi hujumuisha jumla ya shughuli zote za mawasiliano ambazo ni pamoja na: usemi, muktadha na sheria za kufasiri ujumbe (Taylor, 2001).

Uchanganuzi makinifu wa diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz* ulizingatia elementi kuu za diskosi kama zinavyobainishwa na Taylor (ametajwa), hapo juu ambazo ni pamoja na: Usemi ukifasiriwa kama mawasiliano ya kiisimu ambayo huwasilisha maana ya kisemantiki kupitia kwa maandishi au mazungumzo (Leech & Short, 1981). Muktadha ambaeo ulirejelewa katika utafiti huu ukiwa ni wa vijana walio hadhira lengwa na mtagusano wao na jamii kwa jumla katika kipindi mahususi cha kihistoria katika jamii.

Kwa mujibu wa Van Dijk (1977), muktadha huathiri michakato ya diskosi ambapo athari za muktadha hubainika katika diskosi. Kulingana na Fairclough (2000), dhana ya michakato ya kijamii hudhihirisha mshabaha baina ya miundo ya kijamii na mtagusano wa kijamii. Hatimaye, sheria za kufasiri; ufasiri wa diskosi hii ulijifunga katika mazoea ya kijamii. Kwa mujibu wa Fairclough (1995), uchanganuzi makinifu wa diskosi husawiri michakato ya mazoea ya kijamii katika diskosi na kama michakato mingine ya jamii ni zao la muungano na mwingiliano wa elementi za maisha ya jamii ambaeo hubainisha diskosi. Elementi za diskosi zinazobainishwa na Taylor (ametajwa), zilizingatiwa kwani diskosi hii ni zao la michakato ya mitagusano baina ya vijana na jamii (Blommaert, 2005).

Uchanganuzi wa diskosi huchunguza maana katika usemi zaidi ya kiwango cha sentensi kwa kuzingatia muktadhana sheria za kufasiri lugha (Habwe, 1999). Upande mwingine, Bhatia (2013), anasema kuwa uchanganuzi makinifu wa diskosi ni ufichuzi wa itikadi na miundo fiche ya mamlaka kwenye mifumo ya kijamii, kisiasa na

kitamaduni. Hivyo matumizi mabaya ya mamlaka, hegemoni na ukosefu wa usawa hudhihirika kupitia kwa mitagusano ya jamii na hufichama kwenye lugha ya kuvutia na matumizi ya msamiati wa adabu (Van Dijk, 2002).

Baadhi ya masuala yaliyochunguzwa katika utafiti huu ni namna matumizi ya mamlaka, hegemoni na ukosefu wa usawa ulivyodhihirika kupitia kwa mikakati ya kukuza muwala, mazoea ya kijamii na mahusiano ya uwezo. Kwa mujibu wa Fairclough na Wodak (1997), diskosi haizalishwi wala kueleweka bila ya uzingatifu wa muktadha wa matumizi. Diskosi ya *Shujaaz* haitumiki katika ombwe tupu bali huwajibika katika miktadha mbalimbali ambayo ni pamoja na: Kisiasa, kitamaduni, kisaikolojia na kiuchumi. Ina maana kuwa diskosi hii ni mchakato wa kijamii, hasa katika muktadha wa vijana nchini Kenya (Kale, 2003).

Diskosi kama michakato mingine ya kijamii hufungamanishwa na miktadha ya kihistoria ambapo mahusiano ya uwezo huzaliwa au hugombewa na jinsi maslahi hayo hulindwa. Hujibu maswali kuhusu maslahi yanayohusisha diskosi na kinyang'anyiro cha mahusiano ya uwezo (Janks, 1997). Mfano wa maswali yaliyomwongoza mtafiti katika kutafitia diskosi ya *Shujaaz* ni pamoja na: Je, diskosi hii iliwasilishwa au ilijiwasilisha vipi? Ni maslahi ya nani yaliyolindwa na uwasilishaji wa aina fulani? Ni maslahi ya nani yaliyotelekezwa? Athari ya uwasilishaji huo kwa vijana? Ifahamike kuwa diskosi hii ni mali ya jamii na hutekeleza wajibu wake kulingana na maslahi ya makundi yenye uwezo (Fairclough, 1995).

Maswali katika aya iliyotangulia ni thibitisho kuwa uchanganuzi makinifu wa diskosi ni taaluma ya kimsingi inayotoa majibu yanayohusishwa na uhusiano baina ya lugha, jamii, mamlaka, utambulisho, itikadi, siasa na tamaduni za jamii. Mapitio ya maandishi yilibainisha kuwa kumekuwepo na juhudi za wataalamu mbalimbala kutafitia diskosi tofauti tofauti kama mchakato wa kijamii. Chandler (2013), alitafitia *Memes* kwenye mitandao ya kijamii na kupata kwamba uchanganuzi makinifu wa diskosi huhusishwa na changamoto za kijamii kwa nia ya kuleta mageuzi. Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa *Memes* maarufu katika mitandao ya kijamii zilichapishwa katika jarida hili. *Memes* ziliwaelekeza vijana katika kufanya maamuzi, kushiriki

katika shughuli za kijamii na namna ya kuhusiana na wanajamii wengine na zilikusudiwa kuwaelimisha vijana kupitia kwa burudani.

Mitandao ya kijamii; *Facebook*, *Twitter*, *WhatsApp*, *Instagram*, *You Tube* na matumizi ya arafa ilifanikisha mawasiliano baina ya *Shujaaz* na vijana. Mitandao hii ilitumiwa kupata: maoni, ushauri na majibu ya maswali yaliyoulizwa. Lilikuwa jukwaa la kueleza hatua ambazo vijana wangechukua ikiwa wangejipata katika hali kama iliyo hadithini. Hadithi hizi zilisisitiza mielekeo mahususi (Vartanova, 2008), katika maisha ya vijana. Diskosi hizi zilihakiki mabadiliko ya kijamii na kisiasa katika jamii. Kwa mujibu wa Colebatch (2003), vikatuni vya mashujaa humpa msomaji mwelekeo wa hulka njema. Wahusika mashujaa katika data ya utafiti huu walifanya maamuzi ya kawaida na yasiyokuwa ya kawaida katika hali ya uhalisia. Maamuzi ambayo yaliwafahamisha vijana kuhusu masuala mbalimbali katika jamii.

Karikari (2016), alitafiti kuhusu diskosi za ajira ya watoto nchini Ghana na kupata kwamba ajira ya watoto ni changamoto iliyokithiri katika mataifa yanayoendelea. Kwa mujibu wa Fairclough (1992), diskosi huangazia changamoto za kijamii. Changamoto zilizowakumba vijana katika data ya utafiti huu ni pamoja na: ukosefu wa ajira, mimba za mapema, matumizi ya dawa za kulevyta na walimu kutohudhuria vipindi vya masomo skulini. Hatimaye, Habwe (1999), alijikita katika matatizo ya muwala na maana ya kipragmantiki katika hotuba za wanasiasa. Mada kama mkakati wa kukuza muwala, sauti za kionomatopeya na maandishi panelini ni baadhi ya vipengele vilivyokuza muwala katika sampuli ya utafiti huu.

Tafiti za wataalamu hawa hapo juu kuhusu diskosi kama mchakato wa jamii zilidhahirisha kuwa dhana ya mchakato wa kijamii huweka wazi mshikamano baina ya miundo na mitagusano ya kijamii katika diskosi (Fairclough, 2000). Mapitio ya maandishi yalibainisha pengo lililopo katika uchanganuzi makinifu wa diskosi hasa katika vikatuni. Utafiti huu ulilenga kuziba pengo hili kwa kuchanganua kimakinifu diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz*.

Vikatuni, lugha ya ishara na istilahi zilizoandikwa hurejelea dhana moja (Eisner, 1985). Wazo hili linashadidiwa na Neil (2012), anaposema kuwa michoro ya picha si

utanzu wa sanaa bali ni lugha inayokua. Paneli zenyе michoro ya picha hupangwa kwenye msuko ili kuunda lugha ya “kutazamwa”. Vikatuni ni zao la uandishi na uchoraji na hutumiwa kuwasilisha kazi ambazo zinaweza kutafitiwa kiisimu jinsi ilivyo katika utafiti huu (Neil, 2012). Vikatuni kivyake si lugha ila huandikwa kwa lugha ya kutazamwa kama ilivyo katika riwaya na magazeti.

Dhana ya vikatuni inafasiriwa na McCloud (1993), kuwa ni michoro ya picha iliyopangwa pamoja katika msuko ili kupidisha maarifa au kuzua ujumi. Fasiri hii haijakamilika kwa sababu ilitenga kazi zilizowasilishwa kwa michoro ya picha iliyambatanishwa na maandishi (Neil, 2005). Mfano wa kazi ambayo michoro ya picha huambatanishwa na maandishi ni diskosi ya *Shujaaz*. Isitoshe, fasiri hii ilipuuza vikatuni vilivyowasilishwa kwa paneli moja na kuviondoa katika ulimwengu wa vikatuni. Hii ni kwa sababu vikatuni hivi havina msuko. McCloud (ametajwa) alipuuza wazo kuwa paneli moja inaweza kusimulia hadithi na kujisimamia bila kutegemea elementi nyingine.

Mjadala kuhusu dhana ya vikatuni kulingana na Boyd (2015), husheheni hoja tatu: Kwanza, msuko; michoro ya picha zilizopangwa kwenye paneli zaidi ya moja ili kujenga mtiririko wa hadithi. Msuko ni tofauti kuu iliyopo baina ya vibonzo na vikatuni. Vibonzo husimulia hadithi kwa paneli moja ilhali msuko wa vikatuni hukuzwa kwa paneli mbili au zaidi. Pili, michoro ya picha; vikatuni lazima viwe na michoro ya picha. Michoro hii hupambanua maana ya maandishi panelini (Piro, 2002). Hatimaaye, maandishi hukamilisha vikatuni. Maandishi ni kipengele kinachoendeleza mwingiliano baina ya michoro ya picha na msuko wa hadithi (Nortion, 2003). Michoro ya picha huambatanisha na maandishi ambayo huwa vipashio vikubwa kama vile mofu, maneno, virai, vishazi na sentensi. Vipashio hivi vilipangika kwa njia spesheli ili kufanikisha mawasiliano katika sampuli ya utafiti huu.

Usuli wa mfumo wa ukuaji wa muundo wa vikatuni ulimwenguni unahuishwa na kuvumbuliwa kwa taaluma ya uchapishaji (McCloud, 1993). Mwanzo wa uchapishaji wa vikatuni ulimwenguni kama anavyosimulia Scott (2011), unahuishwa na Mwingereza Willam Hoggarth. Kutokana na kazi yake ya kejeli iliyochapishwa katika

machapisho sita mnamo mwaka wa 1731 ambayo yalisomwa kwa awamu. Raia wa Uswizi, Rodolphe Topffer mnamo mwaka wa 1840 aliambatanisha maandishi na michoro ya picha. Hali hii ilikuwa kichocheo kikubwa katika kuafikia muundo wa sasa wa vikatuni.

Sampuli ya utafiti huu ilitokana na jarida la *Shujaaz* linalowasilishwa kwa msimbo wa Sheng. “*Shujaaz*” ni istilahi yenyе maana sawa na dhana “mashujaa” katika Kiswahili Sanifu. Msimbo huu hufanikisha mawasiliano mionganı mwa vijana na unadaiwa kuzuka katika miaka ya sitini na sabini kwenye mitaa ya mapato duni ya Eastlands, jijini Nairobi (Abdulaziz & Osinde, 1997). Wataalamu hawa wanadai kuwa msimbo wa Sheng uliibuka katika hali ya mwingiliano wa lugha mbalimbali nchini Kenya. Huu ni msimbo wa kijamii utumiwao na vijana kwenye mawasiliano katika maeneo ya mashambani na mijini (Mbaabu, 1996). Umesambaa katika sehemu mbalimbali nchini Kenya kutokana na matumizi yake katika vyombo vyaya habari na mawasiliano mengine.

Vilevile diskosi ya *Shujaaz* ni dhihirisho kuwa vitabu, majarida au makala, magazeti au machapisho mbalimbali yanaweza kuchapishwa kwa msimbo wa Sheng ili kuwafaidi vijana (Mugubi, 2006). Diskosi ya *Shujaaz* huwalenga vijana kuitia msimbo wa Sheng. Msimbo huu ni kitambulisho cha vijana kutokana na umaarufu wake mionganı mwao (Kobia & Kinge'i, 2007). Utafiti uliofanywa na shirika la USAID (2013), ulibainisha kuwa diskosi hii huwapa vijana mshawasha wa kushiriki katika masuala ya kisiasa na kijamii. Huboresha maisha kwa kubadili mielekeo, uhamasishaji na kuendeleza hulka njema mionganı mwao.

Jarida hili huchapishwa na kampuni ya *Well Told Story* kuanzia Februari, 2010 na huchapishwa mara moja kwa mwezi. Ndani mna michongoano, hotuba, tawasifu, habari kutoka mitando ya kijamii na tamthilia inayoigizwa kwa njia ya michoro ya picha. Malengo makuu ya jarida hili ni kuburudisha na kuwaelimisha vijana kuhusu uongozi, kuanzisha na kuendeleza biashara, elimu ya afya ya uzazi na kilimo. Vikatuni hivi vilibainika kuwa njia ya kipekee ya kisasa ya usimulizi wa hadithi. Vilisheheni utamaduni pendwa. Jarida hili hutolewa bure.

Utafiti uliofanywa kuhusu *Shujaaz* ni pamoja na utafiti wa Ngugi (2017), uliojikita katika taaluma ya fasihi. Jarida hili likichukuliwa kuwa nyenzo ya fasihi lina thamana ya kukuza na kuendeleza masuala mbalimbali kuhusu maisha ya vijana (Ngugi, 2007). Ni kutokana na upanuzi wa msimbo wa Sheng na kutumika katika uwasilishaji wa jarida hili, kulenga hadhira ya vijana, kuwasilishwa kwa kutumia michoro ya picha, kufadhiliwa na wadhami ndipo utafiti huu ulilenga kuchanganua kimakinifu diskosi ya *Shujaaz*.

1.2 Suala la Utafiti

Licha ya ukweli kuwa vikatuni vimechapishwa kwa kipindi cha takribani karne mbili, utafiti kuvihusu umeanza kutiliwa maanani katika miaka ya sabini barani Uropa na miaka ya themanini katika eneo la Afrika Mashariki. Tafiti kuhusu mada ya vikatuni zimezidi kukubalika kwa upana katika nyanja za kiusomi. Diskosi ya *Shujaaz* kama aina nyingine ya diskosi ina matumizi maalumu ya lugha na uteuzi wa kipekee wa msamiati uliolenga hadhira ya vijana. Uteuzi ambao huashiria mwelekeo wa mwandishi kuhusu mada mbalimbali. Tafiti za awali katika vikatuni vya *Shujaaz* zilishughulikia mawanda ya fasihi na elimu ya afya. Hata hivyo, zimepungukiwa kwa kukosa kuchanganua kimakinifu diskosi ya vikatuni. Utafiti huu uliazimia kufidia upungufu huu kwa kuangazia uchanganuzi makinifu wa diskosi katika vikatuni vya *Shujaaz* na ulijikita katika muwala, mikakati ya mazoea ya kijamii na mahusiano ya uwezo.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

- i. Kueleza namna muwala ulivyokuzwa katika diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz*.
- ii. Kufafanua mikakati ya mazoea ya kijamii katika diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz*.
- iii. Kutathmini jinsi mahusiano ya uwezo yalivyowasilishwa katika diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz*.

1.4 Maswali ya Utafiti

Maswali yaliyojibwa na utafiti huu ni:

- i. Je, muwala hukuzwa vipi katika diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz*?

- ii. Ni mikakati ipi ya mazoea ya kijamii iliyotumiwa kuwasilisha diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz*?
- iii. Mahusiano ya uwezo hudhihirika vipi katika diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz*?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Taaluma ya isimu inafaidika na utafiti huu, kwa sababu matokeo ya utafiti huu ni nguzo muhimu katika kuchangia maarifa ya wanafunzi, walimu wa lugha na wataalamu wa isimu katika kuangazia wajibu wa lugha kama njia mbadala ya kusuluhisha changamoto zinazowakumba wanajamii hususan makundi maalumu kama vile vijana. Pia, utafiti huu ulilenga kuthibitisha namna uwezo unavyodhihirika kupitia kwa lugha kama chombo cha kudhibiti makundi mbalimbali. Hatimaye, utafiti huu uliazimia kutathmini mikakati ya mazoea ya kijamii inayotumiwa na wenye uwezo kupitia kwa lugha au msimbo teule ili kujitambulisha na makundi maalumu katika jamii.

1.6 Upeo wa Utafiti

Jarida la *Shujaaz* huchapishwa na kampuni ya *Well Told Story* na aghalabu huwasilishwa kwa msimbo wa Sheng. Kipindi kati ya 2010-2018 kiliteuliwa kwa sababu kimeshuhudia matukio maalumu yaliyodhihirisha mahusiano ya uwezo nchini Kenya. Kwa mujibu wa Blommaert (2005), upeo wa utafiti unaohusu uchanganuzi makinifu wa diskosi huangazia athari za mahusiano ya uwezo katika diskosi iliyozaliwa katika muktadha maalumu. Aidha, aina ya data iliyokusanywa ilijumuisha maandishi na michoro ya picha. Michoro na ishara nyingine zilizingatiwa kwa sababu uchanganuzi makinifu wa diskosi haujikiti tu katika ujumbe uliowasilishwa kwa maandishi ila hushughulikia ishara za kisimiotiki kama vile michoro ya picha na ishara maalumu katika diskosi teule (Van Dijk, 1995).

1.7 Maelezo ya Istilahi

Istilahi muhimu zilizotumika katika utafiti huu ni:

- Diskosi:** Hadithi inayosimuliwa kwa michoro ya picha iliyoambatanishwa na maandishi ili kuwasilisha ujumbe katika muktadha maalumu wa vijana.
- Kijana:** Mtu wa jinsia ya kike au kiume mwenye umri baina ya miaka kumi na miwili na miaka thelathini na mitano ambaye ni msomaji au mhusika katika *Shujaaz*.
- Paneli:** Sehemu ambayo picha ya michoro ya vibonzo au kibonzo hupatikana. Hivyo, ni msingi wa kujenga maana katika diskosi ya vikatuni. Paneli mbili au zaidi zinapokaribiana hujenga msuko. Aghalabu kila ukurasa huwa na paneli sita.
- Sheng:** Msimbo unaozungumzwa nchini Kenya ambao huchanganya lugha ya Kiswahili, Kiingereza na lugha za kiasili kama vile Kikuyu na Kidholuo.
- Shujaaz:** Ni jarida linalowasilishwa kwa michoro ya picha iliyoambatanishwa na maandishi na kuchapishwa na kampuni ya *Well Told Story* kuanzia Februari, 2010.
- Uwezo:** Maslahi ya wadhamini na mwandishi yaliyodhahirika kupitia mada mbalimbali katika *Shujaaz*.
- Kibonzo:** Mchoro au michoro ya picha kwenye paneli moja ambayo hukusudia kusimulia hadithi kwa kuchekesha na aghalabu huambatanishwa na maandishi.
- Vikatuni:** Kundi la michoro ya picha kwenye paneli zaidi ya moja ambayo inasimulia hadithi na maandishi kama maelezo ya michoro ya picha hizo.
- Usemi:** Ujumbe uliowasilishwa katika jarida la *Shujaaz* kupitia kwa maandishi au michoro ya picha au yote kwa pamoja.

MWAUO WA MAANDISHI

2.1 Dhana ya Vikatuni

Diskosi husheheni maarifa na kumbukumbu za michakato ya kijamii (Van Dijk, 1998). Wakati wa vita, mipaka ya kejeli huwa baina ya “sisi” dhidi ya “wao”. Vikatuni huwa havikuzi tu mgawanyiko wa kisiasa bali huwa kitambulisho cha taifa (Streicher, 1967). Scott (2011), alitafiti kuhusu vikatuni na ukosefu wa amani na kupata kwamba dhima ya vikatuni kuwa ya kuburudisha na kufahamisha katika kipindi cha vita. Viliburudisha nyakati za huzuni, kupigania amani na demokrasia. Utafiti wa Scott (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kuchanganua diskosi ya *Shujaaz* katika kipindi maalumu cha kihistoria. Pia, kufafanua namna deiksisi nafsi ziliwasilisha maslahi ya “sisi” dhidi ya “wao”. Tofauti ni kuwa utafiti wa Scott (ametajwa), ulihusisha sampuli ya vikatuni vilivyochapishwa nchini Marekani ilhali sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kutoka vikatuni vinavyochapishwa nchini Kenya.

Aidha, diskosi huangazia uwezo, mamlaka na ukosefu wa usawa na namna hali hizi husambazwa au kukataliwa na makundi ya kijamii (Van Dijk, 1995). Smith (2012), alichunguza jinsi matumizi ya ishara ya “Nyota ya Daudi” katika vibonzo vilivyochapishwa katika vyombo vya habari ulimwenguni. Hii ni baada ya nchi ya Israeli kushambulia meli ya kupeleka msaada eneo la Gaza katika Taifa la Palestinia tarehe 31/05/2011. Tukio hili lilichangia ubaguzi wa rangi na kukejeliwa kwa Wayahudi wanaoishi katika maeneo mbalimbali ya dunia. Utafiti wa Smith (ametajwa), ulibainisha kuwa kukosolewa kwa nchi ya Israeli kupitia vibonzo kulivuka mipaka na kueneza uchochezi na chuki dhidi ya Wayahudi. Masuala aliyoyaangazia ni ubaguzi wa rangi, umwagikaji wa damu, mashetani, unafiki, mauaji ya kimbari na pesa. Utafiti wa Smith (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kuangazia namna ishara za kisimiotiki zilivyotumiwa kuwasilisha masuala ambayo ni mwiko katika *Shujaaz* kwa njia ya kijazanda. Utafiti wa Smith (ametajwa), ulihusu takribani magazeti yote ulimwengu ambayo yalichapisha vibonzo mtandaoni kuhusu kushambuliwa kwa meli ya kupeleka msaada katika eneo la Gaza ilhali utafiti huu ulihusu jarida la *Shujaaz* linalohusu masuala la vijana nchini Kenya.

Baadhi ya vipengele vinavyoshughulikiwa katika uchanganuzi makinifu wa diskosi ni balagha (Wodak & Meyer, 2008). Mwetulundila na Kangira (2015), walichunguza

matumizi ya balagha na ucheshi katika vibonzo vya kisiasa nchini Namibia. Wanadai kuwa vibonzo huvutia wakati mchoraji anapochora vibonzo vya ucheshi ambavyo ujumbe wake huwa kinyume na matarajio ya msomaji kupitia mbinu ya anwani, semi, chuku, ishara za michoro ya kisimiotiki, lakabu, matumizi ya maneno yaliyokolea wino, tanakuzi, jazanda, kinaya, semi, toni na matumizi ya alama ya hisi. Utafiti wa Mwetulundila na Kangira (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kutambua mkakati wa kukejeli maovu kupitia kwa matumizi na mikakati ya mazoea ya kijamii kama vile jazanda na unominishaji. Tofauti ni kuwa, utafiti wa Mwetulundila na Kangira (wametajwa), ulitumia sampuli ya magazeti yote yaliyochapishwa mwaka wa 2012 nchini Namibia ilhali utafiti huu sampuli yake iliteuliwa kutoka jarida la *Shujaaz*, nakala zilizochapishwa kati ya miaka ya 2010-2018.

Viongozi wa kiimla katika historia ya binadamu huwadhibiti, huwatimua au hata kuwaua wanavibonzo wanaowakejeli (Scott, 2007). Otuoma (2015), alitafiti kuhusu uchanganuzi wa mtindo na maudhui katika vibonzo vya mhariri katika gazeti la *Taifa Leo*. Utafiti wake ulibainisha kuwa vibonzo vya mhariri huwasilishwa kupitia kwa kejeli, kinaya, na jazanda. Maudhui ya ufisadi, ukabila, ukosefu wa usalama, elimu, uchumi na kazi na siasa hutamalaki. Mahusiano ya uwezo yalidhihirika kupitia maudhui kama vile ufisadi, ukabila, elimu, uchumi na siasa. Utafiti wa Otuoma (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kueleza hatua za kufafanua jazanda katika paneli kulingana na muktadha wa kijamii. Utafiti wa Otuoma (ametajwa), hata hivyo sampuli yake ni kutoka gazeti la *Taifa Leo* ilhali sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kutoka jarida la *Shujaaz*.

Diskosi yoyote ile ni mali ya jamii na hutekeleza wajibu wake kutegemea matarajio ya kijamii ambamo imezaliwa (Fairclough, 1992). Amukowa (2017), alitafiti kuhusu mchango wa vikatuni vya *Kiriku* katika makuzi ya fasihi ya watoto. Baadhi ya dhima ya *Kiriku* aliyoshughulikia ni kuelimisha na kutoa mwelekeo wa; kifalsafa, kiitikadi, kiuchumi na siasa. Utafiti wa Amukowa (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kuangazia mahusiano ya uwezo ambayo hukuza itikadi. Utafiti wa Amukowa (ametajwa), hata hivyo ulihusu vikatuni vya *Kiriku* vinavyowasilishwa kwa Kiswahili Sanifu ilhali utafiti huu ulihusisha sampuli ambalo huwasilishwa kupitia kwa msimbo wa Sheng.

2.2 Matumizi ya Lugha katika Vikatuni

Uchanganuzi makinifu wa diskosi haujifungi tu katika usemi bali hushughulikia masuala ya kisimiotiki kama vile matumizi ya viziada lugha, picha, filamu, sauti na muziki (Van Dijk, 1995). Beck (1999), alitafiti kuhusu vikatuni katika Kiswahili au Kiswahili katika vikatuni? Utafiti wake uliangazia ishara za kipekee za lugha zilizowakilisha sauti za kionomatopeya, historia ya vikatuni katika Afrika Mashariki, usomaji, msuko, muundo wa paneli, usimulizi na utamaduni katika vikatuni. Utafiti wa Beck (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kuangazia sauti za kionomatopeya kama mkakati wa kukuza muwala. Aidha, namna ya kufafanua ishara maalumu katika vikatuni. Utafiti wa Beck (ametajwa), ulihusu vikatuni mbalimbali katika Afrika Mashariki kufikia mwaka wa 1999 ilhali sampuli ya utafiti huu ilichapishwa mara ya kwanza mwaka wa 2010.

Kwa mujibu wa Fairclough (2006). Diskosi ni mchakato wa kuwasilisha, kuashiria, kuunda na kujenga ulimwengu kimaana. Dallacqua (2012), alitafiti kuhusu matumizi ya lugha katika vikatuni na katika utafiti wake alibainisha kuwa mbinu za sanaa kama vile usimulizi katika nafsi ya kwanza, kubadilika kwa rangi ya paneli, tadmini, istiari, mazaji, mbinu rejeshi, kisengere mbele na matumizi ya lugha ya msimbo. Utafiti wa Dallacqua (ametajwa) ulifaa utafiti huu katika kueleza matumizi ya msimbo wa Sheng katika muktadha wa vijana kama tukio la kijamii. Tofauti ni kuwa utafiti wa Dallacqua (ametajwa), ulihusisha sampuli kutoka vikatuni vya Marekani ilhali sampuli ya utafiti huu huchapishwa nchini Kenya.

Aidha, diskosi huundwa na jamii, matumizi ya lugha huamuliwa kijamii na lugha hubadilika kulingana na hali ya jamii (Fairclough, 2006). Belhassena (2014), alitafiti kuhusu vipengele vya mtagusano wa lugha mbalimbali katika vikatuni vya Taifa la Algeria katika *Sabaous Houna Fighter* na alipata kwamba kuwasilishwa kwa vikatuni hivi katika msimbo ulitegemea: shinikizo la kijamii, chombo cha kuangazia masuala ya kijamii na kusambaza kaida za kijamii. Utafiti wa Belhassena (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kuangazia matumizi ya msimbo wa Sheng mionganoni mwa vijana kuwa mchakato wa kijamii. Kupitia kwa msimbo huu *Shujaaz* hutekeleza wajibu wa kuelimisha na kuburudisha. Tofauti ni kuwa utafiti wa Belhassena (ametajwa),

ulihusu sampuli kutoka vikatuni vya *Sabaous Houna Fighter* ilhali sampuli ya utafiti iliteuliwa kutoka jarida la *Shujaaz*.

Uchanganuzi makinifu wa diskosi hutoa sababu zinazofanya diskosi kukubaliwa katika jamii jinsi zilivyo (Fairclough, 1995). Msimbo wa Sheng hutawala diskosi za vijana na watoto katika viwango vyote vya elimu kuanzia chekechea, msingi, sekondari na vyuo vikuu (Githiora, 2002). Ngugi (2017), alitafiti kuhusu fasihi katika lahaja ibukizi, mifano kutoka chapisho la *Shujaaz*. Aliangazia jarida hili kama nyenzo ya kusomwa kifasihi. Baadhi ya maudhui katika *Shujaaz* ni pamoja na: uwajibikaji na kuhimiza vijana kutia bidii maishani. Utafiti wa Ngugi (ametajwa), ulifaa katika kutathmini ni kwa namna gani baadhi ya maudhui yalivyokuza dhamira ya jumla katika diskosi ya *Shujaaz*. Utafiti wa Ngugi (ametajwa), hata hivyo uliegemea taaluma ya fasihi ilhali utafiti huu ulijikita katika taaluma ya isimu katika kiwango cha uchanganuzi makinifu wa diskosi. Utafiti huu ulijikita katika muwala, mikakati ya mazoea ya kijamii na mahusiano ya uwezo.

2.3 Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi katika Matini

Mkakati wa mazoea ya kijamii hutumiwa katika kutafitia jazanda kama ilivyobainika katika Kobia (2008). Aliyetafiti jazanda zilizotumiwa kusawiri ugonjwa wa UKIMWI katika lugha ya Oluluhyia kama mazoea ya kijamii. Baadhi ya istilahi za kijazanda zilizobainishwa na Kobia (ametajwa) ni ajali, janga, safari na wanyama. Utafiti wa Kobia (ametajwa), ulikuwa dira katika kufafanua jazanda kama mkakati wa mazoea ya kijamii katika utafiti huu. Kuhusisha michoro ya picha ya kijazanda na muktadha wa utamaduni wa jamii lugha. Utafiti wa Kobia (ametajwa), ni tofauti na huu kwani sampuli ni kutoka jamii ya Oluluhyia ilhali sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kutoka vikatuni vya *Shujaaz*.

Uchanganuzi makinifu wa diskosi huchunguza matumizi ya lugha katika miktadha ya kijamii (Schiffrin, 1988). Musolf (2012), alitafiti kuhusu lugha ya kimafumbo kama sehemu ya uchanganuzi makinifu wa diskosi katika kupeleleza na kubainisha lugha iliyoeneza ubaguzi wa rangi nchini Uswizi. Alibainisha kuwa mkakati wa uchanganuzi makinifu wa diskosi hufaa katika kufasiri lugha yenye maana tata za kimafumbo katika muktadha wa ubaguzi wa rangi. Utafiti wa Musolf (ametajwa),

ulifaa katika kuchanganua utata wa kimaana kama mazoea ya kijamii. Hii ni kwa sababu uchaganuzi makinifu wa diskosi ni uchanganuzi wa lugha katika uamilifu wake na uchanganuzi huu hauwekewi mipaka ya kiisimu katika kuhusisha uamilifu wa lugha na shughuli za binadamu (Brown & Yule, 1983). Hata hivyo, utafiti wa Musolf (ametajwa), ulihusisha hotuba, taarifa ya habari, matangazo ya biashara, fasihi, siasa na sayansi nchini Uswizi ilhali utafiti huu sampuli yake iliteuliwa kutoka vikatuni.

Diskosi huangazia changamoto za kijamii (Fairclough, 1995). Duanprankhon (2012), alitafitia uchanganuzi makinifu wa diskosi katika anwani za taarifa ya habari katika vyombo vya habari kuhusu uhalifu ulioteklezwa na vijana katika nchi ya Thailand. Baadhi ya masuala aliyoangazia ni pamoja na: ujambazi na maisha ya mjini, alibainisha kwamba uhalifu nchini Thailand hutekelezwa na vijana kati ya umri wa miaka 18 hadi 25. Aliangazia anwani zilizotumiwa na vyombo vya habari kama suala la mazoea ya kijamii ambayo huathiri mielekeo ya wasomaji wake kuhusu uhalifu mijini. Isitoshe, aliangazia uzalishaji wa usemi na mhariri kama mchakato wa kijamii ambao hulinda maslahi ya wenyewe uwezo katika jamii. Utafiti wa Duanprankhon (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kuangazia mahusiano ya uwezo baina ya makundi mbalimbali. Utafiti wa Duanprankhara (ametajwa), ulihusu sampuli kutoka vyombo vya dola nchini Thailand.

Lugha kama chombo kinachounda jamii haiwezi kujitenga na itikadi (Van Dijk (1998). Sardabi, Biria na Azin (2014), walitafiti kuhusu hotuba ya Rais wa nchi ya Iran, Hassan Rouhan katika mkutano wa sitini na nane wa Baraza la Umoja wa Mataifa mnamo mwaka wa 2013. Waligundua kuwa Rais Rouhan alikuwa na mtazamo tofauti akilinganisha na Marais waliomtangulia katika Taifa la Iran. Rais Rouhan alijiwasilisha kuwa bora kuliko marais waliomtangulia kuhusu uhusiano wa nchi ya Iran na mataifa ya Kimagharibi. Utafiti wa Sardabi, Biria na Azin (wametajwa), ulifaa utafiti huu katika kueleza namna makundi yenye uwezo huwasilisha maslahi yao kupitia kwa *Shujaaz* ili kueneza itikadi yao. Utafiti huu ni tofauti na utafiti wa Sardabi, Biria, na Azin (wametajwa), kwa sababu sampuli ya utafiti wao ilihusu hotuba ya Rais Rouhan katika mkutano wa 68 wa Baraza la Umoja wa Mataifa.

Uchanganuzi makinifu wa diskosi hufafanua diskosi kama mchakato wa kijamii na huangazia diskosi katika kujikita kwa vipashio vya kiisimu na diskosi kama mazoea ya kijamii (Faircough, 1992). Matara (2014), alitafiti kuhusu uchanganuzi wa lugha ya amani na maridhiano katika muziki nchini Kenya (2008-2012). Katika utafiti wake msisitizo uliwekwa kwenye vipashio vya kiisimu pamoja na uchanganuzi wa diskosi kama mchakato wa kijamii. Baadhi ya maudhui aliyoangazia ni pamoja na Wakenya kuwacha kupigana, ukabila na uchochezi. Utafiti wa Matara (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kuchanganua baadhi ya data ya utafiti huu ambayo iliwasilishwa kwa msimbo wa Sheng. Sawia na utafiti wake utafiti huu ultumia nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi. Tofauti ni kuwa utafiti wa Matara (ametajwa), ulihusu sampuli ya nyimbo ilhali sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kutokana na vikatuni.

2.4 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi ambayo hudokeza kuwa diskosi na jamii hutegemeana na kujengana. Waasisi wa nadharia hii ni pamoja na Wodak (1995), Fairclough (1992, 1995), Fairclough & Wodak (1997), Van Dijk (1997, 2006) na Blommaert (2005). Nadharia hii hutoa sababu zinazofanya diskosi ambazo ni zao la jamii kukubaliwa jinsi zilivyo (Fairclough, 1995).

Fairclough (1992), anasema kuwa uchanganuzi makinifu wa diskosi hutokea kwa namna tatu. Kwanza, uchanganuzi makinifu wa diskosi hujikita katika vipashio vya kiisimu kama vile leksimu, sarufi, muwala na muundo wa diskosi. Mtazamo huu ulifaa katika kuchanganua namna muwala ulivyokuzwa katika diskosi ya *Shujaaz* katika muktadha wa kitamaduni vinamosomwa. Pili, uchanganuzi makinifu wa diskosi hushughulikia diskosi kama mchakato wa kijamii. Hii ina maana kuwa diskosi ni mali ya jamii na hutekeleza wajibu wake kutegemea matarajio ya wanajamii ambamo diskosi hiyo imezalishwa. Hivyo, diskosi ya *Shujaaz* ni tukio la mchakato wa jamii ambalo wajibu wake ni kuelimisha vijana kuitia kwa burudani katika muktadha wa vijana nchini Kenya. Hatimaye, diskosi ya *Shujaaz* ilishughulikiwa kama suala la mazoea ya kijamii. Mtazamo huu ulifafanua kuwa diskosi huzaliwa, husambazwa, huenezwa na kutumiwa katika jamii. Mikakati mbalimbali ya mazoea ya kijamii

hutumiwa kuipa diskosi hii utambulisho katika muktadha wa vijana wanaoishi katika mitaa ya mabanda nchini Kenya.

Nadharia hii hukusudia kudhihirisha namna mahusiano ya kijamii, maarifa au ujuzi, utambulisho wa wahusika na uwezo wa wahusika unavyoundwa katika jamii kupidia diskosi. Mtazamo huu ulipelekea Fairclough na Wodak (1997), kujadili umuhimu wa uchanganuzi makinifu wa diskosi amba ni pamoja na kusaidia katika kushughulikia na kutoa suluhu la changamoto za kijamii. Diskosi huchangia ujenzi wote wa miundo ya jamii ambayo huchangia kuziunda au kuikwamiza kupidia kaida zake, mahusiano, utambulisho pamoja na taasisi zilizosheheni miundo hiyo. Hii ni kwa sababu diskosi ni tendo la kuwakilisha, kuashiria, kuunda na kujenga ulimwengu kimaana (Fairclough, 2006).

Fairclough (2006), anabainisha vipengele vitatu vya kudhihirisha athari za diskosi. Kwanza, diskosi huchangia ujenzi wa utambulisho wa kijamii. Pili, diskosi husaidia katika ujenzi wa mahusiano ya uwezo baina ya watu. Hatimaye, diskosi husaidia katika ujenzi wa mfumo wa maarifa na imani. Mawazo ya Fairclough (ametajwa), yalifaa utafiti huu katika kufafanua mazoea ya kijamii yanayoipa diskosi ya *Shujaaz* utambulisho katika muktadha wa vijana. Aidha, kueleza mahusiano ya uwezo baina ya wahusika, vijana, wadhamini na watu mashuhuri katika jarida hili. Hatimaye, kutathmini namna diskosi ya *Shujaaz* hutumiwa kukuza mfumo wa maarifa na urithishaji wa imani zinazochukuliwa kuwa kweli katika jamii.

Mihimili iliyongoza utafiti huu ni pamoja na: Kwanza, Diskosi huundwa na jamii. Matumizi ya lugha huamuliwa kijamii na lugha hubadilika kulingana na hali ya jamii. Matumizi ya lugha huathiriwa na kuundwa na jamii. Uchanganuzi makinifu wa diskosi ni kutafuta mshikamano baina ya miundo ya kijamii na vipengele vya lugha. Msimbo wa Sheng uliowasilisha *Shujaaz* ni kiwakilishi cha vijana kama kundi la jamii. Matumizi ya msimbo huu katika mkakati wa unominishaji ilibainisha namna ya kuunda diskosi hii ili kukuza mielekeo mbalimbali katika jamii.

Vilevile diskosi husaidia katika kuunda na kubadilisha maarifa, mahusiano ya jamii na utambulisho wa jamii. Mhimili huu ulifaa katika kuchanganua masuala yaliyonua

kuarifu vijana na yaliyodhihirisha mahusiano baina ya diskosi ya *Shujaaz* na vijana. Maarifa, mahusiano na utambulisho wa kijamii katika diskosi hii hudhibitiwa au huundwa upya kwa wakati mmoja.

Aidha, diskosi huundwa na mahusiano ya uwezo na husheheni itikadi. Diskosi ni sababu ya kubainika kwa aina mahususi ya tukio la mazoea ya kijamii ambalo hutekeleza jukumu la kiitikadi. Uchanganuzi wa *Shujaaz* ulidhihirisha namna ya ufasiri na upokeaji wa athari zake huwasilishwa. Mhimili huu hudokeza athari za kijamii katika diskosi. Uwezo huathiri kaida za diskosi kwa kuzipa imani fulani. Mhimili huu ulikuwa nguzo muhimu katika kuchunguza *Shujaaz* katika muktadha maalumu wa kijamii nchini Kenya na namna mahusiano ya uwezo yalivyojenga mielekeo na imani kuhusu masuala mbalimbali kama tabaka la kijamii.

Isitoshe, kuundwa kwa diskosi ni suala kuu katika kinyang'anyiro cha mahusiano ya uwezo. Uchanganuzi makinifu wa diskosi huangazia suala la lugha na mamlaka. Hutazama namna mahusiano ya uwezo hutumiwa na kujadiliwa katika diskosi. Pia, huangazia suala la mamlaka ya diskosi. Uchanganuzi makinifu wa diskosi huamini kuwa uwezo wa kudhibiti na kubadili sheria za mchakato wa mazoea ya kijamii na miundo ya diskosi ni njia ya kupata mamlaka. Kaida za diskosi huathiriwa na jamii kwa namna fulani na udhibiti wa michakato ya uzalishaji wa diskosi ambayo ni njia ya wazi ya kiutawala. Hii ni njia moja ambayo kwayo vikundi vyenye uwezo hutawala jamii au nyanja fulani za kijamii. Mhimili huu ulifaa utafiti huu katika kufafanua namna kupitia mahusiano ya uwezo hudhihirika kupitia kwa wahusika, watu mashuhuri, vijana, wadhamini na uana mahusiano ya uwezo hudhihirika.

Ifahamike kuwa nadharia hii huonyesha jinsi jamii na diskosi hujengana. Diskosi husheheni jamii na utamaduni: Jamii huathiri diskosi kwa namna tatu; uwasilishaji wa ulimwengu, mahusiano ya kijamii baina ya watu na ujitalbulishaji wa nafsi. Mhimili huu ulikuwa dira katika kuangazia diskosi ya *Shujaaz* katika muktadha wa vijana na namna masuala yaliyohusu vijana yalivyoshughulikiwa.

Aidha, diskosi huangazia masuala katika muktadha mahususi wa kihistoria. Diskosi haiwezi kutengwa na muktadha wake. Dhana ya muktadha hujumuisha mwingiliano

wa usemi na maarifa ya kijamii na utamaduni. Vikatuni vya *Shujaaz* kama diskosi yoyote ile vilisheheni matukio ya kihistoria katika kipindi maalumu baina ya Februari, 2010 hadi Disemba 2018. Ilibainika kuwa jarida hili ni muundo wa maarifa na kumbukumbu za mchakato wa kijamii (Van Dijk, 1998).

Pia diskosi huweka wazi changamoto za kijamii. Uchanganuzi makinifu wa diskosi hupendelea masuala ya kijamii ambayo kwa kiwango fulani ni zao la athari ya diskosi. Hulenga kuweka wazi mikakati ya kijamii kwa umma ili lugha isiwe kifaa cha kuwahadaa wenyе mamlaka wanapohitaji mamlaka zaidi. Mhimili huu ulifaa katika kufafanua namna changamoto za kisiasa, kijamii, kisaikolojia na kiuchumi zilizowakumba vijana na namna zilivyoshughulikiwa na wenyе mamlaka katika *Shujaaz*.

Hatimaye, diskosi hujieleza, uchanganuzi makinifu wa diskosi hueleza diskosi kuwa mfumo wa kuelewa hutegemea maarifa ya kiusuli ya kihisia, mielekeo na maarifa. Diskosi hudenguliwa na husawiriwa katika mazingira yake ya kijamii (Fairclough & Wodak, 1997). Hii ni hali ambapo jarida la *Shujaaz* lilihusiana na masuala ya kiitikadi na mamlaka katika jamii linamosomwa. Hatimaye, diskosi ni zao la matendo ya kijamii, uchanganuzi makinifu wa diskosi ni mfumo ambao hulenga kufichua mahusiano ya uwezo. Diskosi ya *Shujaaz* ilirejelewa kama tukio la kijamii na ilitoa mwelekeo kuhusu hulka mbalimbali za kijamii.

Mihimili hii iliongoza utafiti huu katika kueleza muwala, kufafanua mazoea ya kijamii na kutathmini mahusiano ya uwezo wa kijamii. Nadharia hii ilithibitisha namna diskosi ya *Shujaaz* ilivyotumiwa kupata ukubalifu wa kuwasilisha maslahi ya mwandishi na wadhamini kupitia kwa mitazamo ambayo haidhihirishi imani za itikadi moja kwa moja. Mfumo wa kuweka wazi hali hii ulidhihirisha jinsi miundo ya kijamii ilibainisha vipengele vya diskosi na namna diskosi ilithibitisha miundo ya jamii (Faircough, 1995).

SURA YA PILI
SURA YA TATU
MBINU ZA UTAFITI

3.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti ulichukua muundo wa kimaelezo. Muundo wa kimaelezo hutumiwa katika taaluma ya kimaelezo kumpa fursa mtafiti kukusanya taarifa, kuandika mukhtasari na kuwasilisha matokeo (Orodho, 2003). Data ya utafiti huu ni michoro ya picha na maandishi ambayo yalikusanywa na kuchunguzwa kwa makusudio ya kuchanganuliwa ili kutoa matokeo. Utafiti huu ultumia mpango wa kimaelezo katika kuchanganua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti kwa sababu data iliyokusanywa haikuhitaji uchanganuzi wa kitakwimu.

3.2 Uteuzi wa Sampuli

Usampulishaji katika utafiti huu ulikuwa mchakato wa kuteua kundi ndogo kutoka kundi kubwa la nakala za *Shujaaz* zilizotafitiwa ili kuafikia malengo ya utafiti (Kothari, 2009). Kwa mujibu wa Gay (1992), mtafiti huteua sampuli kwa sababu ya kuwepo kwa ufinyu au udhaifu fulani ambao huzuia kutafititia idadi lengwa yote. Ufinyu na udhaifu uliomkumba mtafiti unafafanuliwa na Mugenda na Mugenda (1999), wanaposema kuwa rasilimali na wakati ni vizuizi vikubwa katika kufanya maamuzi kuhusiana na uteuzi wa sampuli.

Mtafiti aliteua kimakusudi jumla ya nakala 35 kwa kuzingatia uchanganuzi wa yaliyomo kuafikiana na maswali ya utafiti kutohana na jumla ya nakala 106. Kiwango cha sampuli iliyoteuliwa kilikuwa takribani asilimia thelathini na tatu nukta tatu ya jumla ya nakala zilizochapishwa katika kipindi hiki. Asilimia ambayo iliafikiana na mawazo ya Mulusa (1990), anapopendekeza kuwa thuluthi ya idadi lengwa inatosha kutumiwa katika kufanya makadirio ya sifa zinazochunguzwa katika utafiti. Mugenda na Mugenda (1999), wanasema kuwa katika mbinu ya kimakusudi, mtafiti huwa na uhuru wa kuteua sampuli zilizo na data iliyohitajika. Mtafiti aliteua nakala moja kwa kila matoleo matatu, kuanzia toleo la kwanza Februari mwaka wa 2010 hadi toleo la Disemba mwaka wa 2018.

3.3 Utafiti wa Maktabani

Kazi hii ilihusu usomaji wa kina maktabani. Data ya kimsingi katika utafiti ilitokana na jarida la *Shujaaz* ambalo huwasilishwa kwa michoro ya picha na maandishi. Bali na nakala za jarida hili, kazi nyingine zenyе mielekeo ya uchanganuzi makinifu wa diskosi na vikatuni kama vile tasnifu, vitabu vya kiada, makala, hotuba, picha na matangazo yalisomwa. Aidha, makala, kuhusu mada ya utafiti huu pamoja na uhakiki wake yalisomwa ili kuelewa vikatuni.

3.4 Ukusanyaji wa Data

Shujaaz ni diskosi ambayo huwasilishwa kwa michoro ya picha ambayo huambatanishwa na maandishi. Hivyo mtafiti alisoma sampuli teule na kudondo matini yaliyowekwa katika kategoria mbalimbali kulingana na maswali ya utafiti kwa kutumia orodha ya ukaguzi kama kifaa cha utafiti. Data ilikuwa ya aina mbili; maandishi na michoro ya picha. Data iliyopatikana kutokana na sampuli teule iliwekwa kwenye makundi matatu makuu kulingana na malengo ya utafiti. Kauli za wahusika, uzungumzi nafsi, sauti za kionomatopeya, maneno ya mwandishi na ujumbe katika mandhari ya paneli katika jarida hili iliwasilishwa kwa maandishi. Maneno, virai na sentensi zilidondolewa kama dondo. Pia, michoro ya picha panelini ilidondolewa ili kuafikia malengo ya utafiti.

3.5 Uchanganuzi wa Data

Utafiti ulitumia njia ya kimaelezo katika kuchanganua data kwa misingi ya nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi. Data iliyopatikana kutokana na usomaji wa sampuli iliyoteuliwa ilichanganuliwa kwa njia ya kimaelezo kwa kuongozwa na malengo ya utafiti huu kiukamilifu. Msamiati wa msimbo wa Sheng ulilinganishwa na jazi na vibadala vyake katika Kiswahili Sanifu. Kwa upande wa uwasilishaji, data zimefafanuliwa kwa kutumia njia za kimaelezo na ilitumika na mtafiti kufafanua namna alivyofikiria na kuhisi kuhusu kitu au jambo fulani (Kothari, 2004). Maana anuwai za maneno ya msimbo wa Sheng yalihusisha na muktadha yalimotumiwa kama anavyopendekeza (Fairclough 1992).

3.6 Maadili ya Utafiti

Kuzingatia maadili katika kazi ya utafiti ni suala muhimu (Kothari, 2009). Utafiti huu ulitilia maanani suala la kimaadili. Hii ndio sababu mtafiti alipata kibali kutoka kwa Chuo Kikuu cha Chuka na Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi. Mtafiti alitambua kazi za wataalamu wengine kwa kuwatambulisha katika nukuu na marejeleo. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kulingana na mihimili ya nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi ili pasiwe na mapendeleo ya kibinagsi. Ili kudumisha heshima ya sayansi ya utafiti, data iliyokusanywa iliandikwa na kuhifadhiwa kila mara. Pindi mtafiti alipokosea katika ukusanyaji na uhifadhi wa data aliwaarifu wasimamizi. Isitoshe, utafiti uliweka wazi matokeo ya utafiti na kupendekeza sehemu ambazo zinaweza kufanyiwa utafiti wa baadaye kuhusiana na mada ya utafiti.

SURA YA NNE
MUWALA KATIKA SHUJAAZ

4.1 Utangulizi

Muwala ni sifa ya kimsingi ya diskosi. Dhana hii hurejelea mfuatano wa matukio kwa utaratibu kiasi kwamba yanakuwa na mshikamano wa mawazo katika diskosi nzima. Utafiti huu ulifafanua dhana ya muwala kuwa kipengele cha kisemantiki kinachofasiri ujumbe katika paneli moja ikilinganishwa na paneli nyingine katika diskosi nzima ya vikatuni. Aidha, muwala ulishughulikia jinsi dhana katika diskosi zilivyohusiana na kuingiliana ili kukuza maana ya jumla ya diskosi. Hatimaye, muwala ulimwezesha msomaji kusoma paneli zinazokuza msuko wala si tu mkusanyiko wa paneli zilizowasilishwa kwa pamoja katika diskosi ya vikatuni.

4.2 Mada na Muwala

Mada ni mapatano baina ya washiriki katika mawasiliano kulingana na mhimili wa umuhimu. Uteuzi wa mada ya diskosi hutegemea kilicho muhimu hapa, kwangu na kwake katika kipindi fulani (Coulthard, 1981). Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa kuna nakala ya #29 yenye hadithi ya mada: “Mtiche Akikosa, Utagwara”. Maswali yaliyoongoza uelewaji wa hadithi hii ni pamoja na: Kwanza, namna mada ilivyochangia uelewaji wa hadithi? Pili, namna mada ilivyokuza muwala? Hatimaye, namna mada ilivyokuza muwala uliotokana na msuko na muwala wa kijumla? Muwala wa kijumla ulikuzwa na maarifa ya kiusuli ya hadhira lengwa kuhusu matukio mbalimbali hadithini (Habwe, 1999).

Muwala ulikuzwa na mada kwa kueleza ni kwa nini paneli zilihusiana kimaana katika kujenga msuko wa hadithi (Brown & Yule, 1983). Tazama kielelezo cha 1:

*Mtiche akikosa? Utagwara!!
Mwalimu akikosa? Utafeli!!*
(Tazama, kielelezo cha 1, *Shujaaz* Chapta #29, ukurasa wa 19)

Muwala wa kijumla ulikuzwa na mada hii ikizingatiwa kuwa baadhi ya hadhira lengwa ni wanagenzi. Huenda wameshuhudia visa vyta walimu kutohudhuria vipindi vyta masomo shuleni. Paneli ya kwanza ilisimulia shughuli walizoshiriki wanafunzi walimu waliposa kuhudhuria kipindi. Matukio yafuatayo yalibainika katika kielelezo cha 1:



Kielelezo cha 1, *Shujaaz* chapta #29, ukurasa wa 19

Utangulizi wa hadithi ni mandhari ya darasani. Wanafunzi walishiriki katika kuchongoana, kulala kwenye dawati, kusimama darasani na kupiga gumzo. Hizi ni athari za walimu kutohudhuria vipindi vya masomo shulen. Paneli ya mwisho (Kielelezo cha 2) isiyokuwa na uhusiano wa ujirani na paneli ya kwanza matukio yafuatayo yalidhiihikira:

Muktadha wa mandhari katika kielelezo cha 2 ni ukumbi wa shule kulikofanyika mkuutano wa wazazi na walimu. Wazazi walitaja sababu za walimu kukosa kuhudhuria vipindi vya masomo kuwa:



Kielelezo cha 2, *Shujaaz* chapta #29, ukurasa wa 23

Mwalimu mwengine anasafirisha bodaboda mchana.
Mwalimu mwengine ni mhudumu wa bodaboda mchana.

Performance imeharibika juu walimu wako biashara mchana.

Matokeo (ya mtihani) yamedorora kwa sababu ya walimu kufanya biashara mchana.

Nilienda M-Pesa mchana mwalimu wa class 3 akaniitisha pesa za hio tuition.

Nilienda kutafuta huduma za *M-pesa* mchana (wakati ambao mwalimu anapaswa kuwa shulenii akifunza) mwalimu wa darasa la tatu akaniagiza pesa za masomo ya ziada.

Ndio! Hata mimi ninaunga mkono hio proposal.

Naam, hata nami ninaunga mkono pendekezo hilo (kupewa uhamisho kwa naibu wa mwalimu mkuu).

Kauli hizi ni maoni ya wazazi kuhusu vichocheo vya walimu kutohuduria vipindi vya masomo. Kwanza, kuna mwalimu ambaye ni mhudumu wa bodaboda badala ya kuwa kazini. Pili, kiwango cha masomo kilididimia kwa sababu ya walimu kushiriki biashara wakati waliopaswa kuwa shulenii. Tatu, walimu wanarandaranda njiani wakiwaitisha wazazi pesa za mafunzo ya ziada. Hatimaye, mmoja wao aliunga mkono pendekezo la naibu wa mwalimu mkuu kupewa uhamisho.

Dhana ya mada baina ya paneli ya kwanza na ya mwisho ilifasiriwa kwa kuzingatia uhusiano wa matukio baina ya paneli hizi mbili. Ingawa, hazipo katika mahusiano ya ujirani. Yaliyomo yalihu mada ya hadithi. Paneli ya kwanza ilitoa athari na ya mwisho ilitoa kiini cha walimu kutohuduria vipindi vya masomo.

Paneli hizi zilihusiana kwa njia spesheli. Kilichoziweka pamoja ni suala la walimu kukosa kuhuduria vipindi vya masomo shulenii. Suala lilosababisha kufeli kwa wanafunzi. Kwa mujibu wa Danes (1974), muwala wa diskosi huathiriwa na mshikamano na mwingiliano wa maudhui yanayochangia kukuza mada kuu. Muwala ulikuzwa na matukio panelini kuwa hizi na uhusiano wa dhana. Dhana hizi zilikuwa na ukweli fulani wa mahusiano ya kimaana na mada kuu ya hadithi (Van Dijk, 1987). Mahusiano ya mada yalikuwa kiini cha paneli hizi kusomeka kama sehemu ya hadithi iliyo kuwa ikisimuliwa. Masuala yafuatayo ni baadhi ya elementi zilizokuza muwala baina ya paneli ya kwanza na ya mwisho:

- i) Hadithi hii iliwasilishwa kuitia diskosi ya *Shujaaz* ambavyo huchapishwa nchini Kenya. Hivyo, matukio katika paneli ya kwanza na paneli ya mwisho yalihu siana moja kwa moja na muktadha wa wanamoishi vijana. Muwala wa

- jumla uliokuzwa ultokana na maarifa ya kiusuli walionayo vijana kuhusu athari na sababu za walimu kutohudhuria vipindi vyatya masomo shulen.
- ii) Wahusika vibonzo kwenye paneli hizi walitumia msimbo wa Sheng ambao ulihusishwa na vijana nchini Kenya. Vijana walijitambulisha na wahusika wanafunzi katika paneli ya kwanza na kuwaona kama wenzao.
 - iii) Wahusika katika paneli hizi ni wazazi, wanafunzi na walimu ambao ni washika dau katika sekta ya elimu.
 - iv) Suala muhimu ni kumulika walimu wasiowajibika kwa kukosa kuhudhuria vipindi vyatya masomo shulen.
 - v) Muktadha wa mandhari ya paneli hizi ni shulen: Paneli ya kwanza ni darasani na paneli ya mwisho ni katika ukumbi wa mikutano ambao ulihusiana moja kwa moja na mada iliyohusu walimu kutohudhuria vipindi vyatya masomo shulen.
 - vi) Elementi nyingine ni kama vile sentensi, nomino na vishazi ambavyo vilihusiana kimaana na mada katika paneli ya kwanza na paneli ya mwisho.

(Habwe, 1999: 186)

Ingawa, paneli ya kwanza na ya mwisho zilisambazwa katika sehemu tofauti za hadithi. Muwala ulichangiwa na elementi zilizounda mshikamano wa mawazo au dhana baina ya paneli hizi. Mwandishi alihakikisha kuwa chochote alichangoangazia kilitimiza kigezo cha umuhimu (Coulthard, 1981), ili paneli zitimiza mahitaji ya muktadha wa kiisumu na kimandhari. Muwala baina ya paneli hizi ulibainika nje ya mipaka ya mfuatano wa namna paneli zilivyofuatana katika hadithi iliyosimuliwa. Ishara panelini zimejengeka kwenye misingi ya kufasiriwa na msomaji kwa kuzingatia uhusiano wa dhana moja na nyingine. Licha ya ukweli kuwa hazipo katika ujirani.

Anavyosema Groensteen (1999), ni kuwa paneli hutagusana kimaana bali si lazima ziwe katika ujirani ila ni paneli zote hadithini. Paneli moja huhusiana na nyingine kwa sababu kila paneli huwepo katika vikatuni kwa kuhusiana na nyingine (Groesteen, 2007). Hata hivyo, baadhi ya paneli hazina uhusiano wa moja kwa moja na mada. Ukosefu wa mshikamano wa kimaana baina ya paneli ulisambaratisha mfumo wa

ukuzaji wa mada kuu ya hadithi (Fries, 1983 katika Wang & Guo, 2014). Tazama kielelezo cha 3:



Kielelezo cha 3, *Shujaaz* chapta #29, ukurasa wa 21


Yanayotendeka panelini hayana uhusiano wa moja kwa moja na mada kuu ya hadithi:

Mwalimu: *Unajua wewe ni mrembo hadi other women wameogopa kuingia hoteli?*

Unajua wewe ni mrembo hadi wanawake wengine wameogopa kuingia mkahawani?

Mama yake Malkia: *Stop it with the flattery.*
Wacha kunihadaa.

Mazungumzo panelini hayaambatani na mahitaji ya mada ya hadithi. Yanalazimu swali, "Je, ni kwa nini yawepo hadithini na kwa muktadha upi?" Mkondo wa mazungumzo baina ya wahusika panelini hayakuzi muwala unaoletwa na msuko wa matukio hadithini. Kimaana paneli hii iko nje ya mada kwa sababu iliangazia masuala ambayo yikitathminiwa kivyake hayakuwa na uhusiano wa moja kwa moja na mada kuu. Mazungumzo baina ya mwalimu na Mama yake Malkia yalikuza muwala wa kijumla. Yalihitaji maarifa ya kiusuli kutoka katika nakala tofauti. Katika nakala ya #100, Malkia anasema (Kielelezo cha 4):



Kielelezo cha 4, *Shujaaz* chapt #100, ukurasa wa 16

...My mum huwa busy kila time so mara most yeye hunipeleka kwa my nyanya. My dad hu-work Saudi Arabia. Anatumanga dooh ya fees lakini huwa hakuji home...


...Mama yangu huwa na shughuli nyingi kila wakati aghalabu hunipeleka kwa nyanya yangu. Baba yangu hufanya kazi nchini Saudi Arabia. (Yeye) hutuma karo lakini huwa haji nyumbani...

Kauli hii iliibua dhana kuwa Mama wa Malkia ni mzazi mtepetevu. Alipuuza kuzungumza na Malkia kuhusu masuala yaliyomhusu kama kijana msichana. Alienda kukutana mikahawani na mwalimu aliyedhani angemchumbia. Huenda, ni kwa sababu mumewe hufanya kazi nchini Saudi Arabia na haji nyumbani. Kwa mujibu wa Van Dijk (2001), nguvu za kushawishi huwekewa msingi na maarifa, habari na mamlaka. Mwalimu alitumia uwezo wa kuwa mwalimu kumshawishi Mama yake Malkia kumlipia mwana wake masomo ya ziada.

4.3 Sauti za Kionomatopeya

Kuwepo kwa sauti za kionomatopeya vikatuni ni hustawisha maana ya picha za michoro “zilizonyama” (McCloud, 1993). Anavyosema Beck (1999), ni kuwa sauti za kionomatopeya si sehemu ya maneno ya mwandishi wala michoro ya picha na hupewa nafasi ndogo panelini. Huungana na michoro ya picha ili kuwasilisha maana isiyowasilishwa kwa maneno au michoro ya picha pekee (Harvey, 2001). Sauti ya kionomatopeya ni neno linaloiga sauti ya kitu fulani (Dofs, 2008). Huwasilisha sauti

ya kitu, kiumbe au hali. Sauti hii huiga, huzalisha au huwakilisha sauti ya kimsingi ya kitu fulani. Tazama kielelezo cha 5, sauti ya kionomatopeya, “KUKURIKOO!!!” ilitumiwa kukuza muwala:



Kielelezo cha 5, *Shujaaz* chapta #61, ukurasa wa 30

Kukurikoo!!! ni sauti iliyoiga sauti ya jogoo anapowika. Sauti hii iliashiria kupambazuka, yaani wakati wa majogoo; kumekucha. Ufasiri huu ultokana na maarifa ya kiusuli ya msomaji kuwa, kuwika kwa jogoo kuliashiria mapambazuko. Brown na Yule (1983), wanasisitiza kuzingatiwa kwa maarifa ya kiusuli katika kufasiri muwala. Panelini sauti hii iliambatana na picha za michoro ya miale ya juu angani na ilitoka kwa nyumba, alikolala jogoo.

Kwa mujibu wa Petersen (2007), kuna uhusiano wa kimaana baina ya sauti ya kionomatopeya na michoro ya picha. Michoro hii hutoa maelezo zaidi katika kujenga maana ya panelini. Sauti hizi zinapochanganuliwa picha za michoro huzingatiwa. Sauti *kukurikoo!!!* iliyaweka matukio panelini na paneli zilizofuatia kwenye kipindi maalumu cha kiwakati. Matukio yalitokea “wakati wa majogoo”, yaani alfajiri na mapema. Maana iliyopatikana ni “siku iliyofuata asubuhi na mapema.” Mhusika Malkia, Kazuri na Jipendo katika paneli zilizotangulia walihudhuria “Disko Matanga” usiku. Hata hivyo, Malkia alikosa kurudi nyumbani pamoja nao. Paneli iliyofuata mhusika Malkia aliamka asubuhi na mapema siku iliyofuata kuwasaka. Kwa mujibu wa Eisner (1985), wakati katika vikatuni hutokana na msuko wa matukio katika

hadithi inayosimuliwa. Sauti hii ililetä mshikamano baina ya paneli zilizotangulia kwa kubainisha wakati ambapo Malkia aliamka kwenda kuwatafuta Jipendo na Kazuri.

4.4 Maandishi katika Mandhari ya Paneli

Kwa mujibu wa Badman (2012), maandishi katika michoro panelini ni sehemu ya mandhari. Maandishi haya husomwa na wahusika kama masimulizi au hata wakayaandika. Maandishi katika mandhari ya paneli yalitoa maelezo yaliyoendeleza msuko wa hadithi. Yalikuza muwala wa hadithi kwa kudhihirisha wakati, mahali, hitimisho la hadithi na mabango ya biashara.

4.4.1 Wakati

Japo si kwa njia ya moja kwa moja maandishi katika mandhari ya paneli yalidhihirisha wakati wa kutendeka kwa tukio. Wakati panelini huwakilisha msuko wa matukio hadithini na huafikiana na matarajio ya msomaji kuhusu msuko wa hadithi (Marion, 1993). Maandishi katika mandhari ya paneli yalikuza muwala uliokuzwa na msuko kwa kubainisha wakati wa tukio fulani. Kwa mfano, kuna mchoro wa basi lilioandikwa “RISING SUN,” kifungu hiki kina maana sawa na “Jua linalochomoza”: Tazama kielelezo cha 6:



Kielelezo cha 6, *Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 11

Muwala uliokuzwa na kifungu hiki kwa namna zifuatazo: Basi kwenye paneli huondoka asubuhi na mapema kuelekea mjini na ndio sababu linaitwa “Rising Sun”. Bango lililopo kando ya barabara lilithibitisha kuwa safari ya kwenda mjini Ingo ni kilomita mia mbili sabini na saba. Huu ni mwendo mrefu ambao ulihitaji basi kuondoka mashambani asubuhi mapema. Paneli zilizotangulia wahusika Charlie Pele

na Taabu walikuwa wamepanga kutazama mechini ya fainali ya michuano ya Taji la Ingo mjini Ingo siku iliyofuata. Pengo lililopo baina ya paneli iliyotangulia na kielelezo cha 6 lilizibwa na matarajio kuwa Taabu na Charlie Pele waliabiri basi hili. Muwala ulikuzwa kupitia kuwa uhusiano wa mshikamano baina ya paneli zilizotabirika kutokana na msuko wa hadithi (Crombie, 1985). Maandishi katika mandhari ya paneli yalidhihirisha wakati watukio hadithini. Ingawa, hayakubainishi wakati moja kwa moja. “Asubuhi na mapema” ilirejelewa kwa kifungu, “Rising Sun”. Basi hili lililinganishwa na juu linalochomoza. Maneno ya mwandishi panelini:

Siku iliyofwata
Siku iliyofuata

Kifungu hiki kililazimu kuzingatiwa kwa paneli zilizotangulia. Kwa mujibu wa paneli iliyofuata hii ndio siku Taabu na Charlie Pele walisafiri kwenda mji wa Ingo. Aidha, bango la barabarani lililoandikwa “Ingo City” panelini ni ushahidi tosha kuwa gari hili halielekei kwingine ila mjini Ingo.

4.4.2 Mahali

Utafiti huu ulibainisha kuwa maandishi katika mandhari ya paneli huashiria mahali tukio lilipotokea. Kwa mujibu wa Marion (1993), baadhi ya elementi ambazo huwezesha uelewaji wa vikatuni ni matarajio ya msomaji katika kujaza mapengo hadithini. Yalibainisha mahali kama vile hospitalini, hemani na shuleni. Tazama kielelezo cha 7:



Kielelezo cha 7, *Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 21

“Youth Tent” ni kifungu cha maneno katika lugha ya Kiingereza chenye maana sawa na “Hema la vijana.” Alama ya mshale chini ya maneno “Youth Tent” iliashiria

mchoro wa hema uliopomkabala na jumba lenye msalaba. Maana ya kifungu hiki hayangekamilika bila ya kuzingatia ishara ya msalaba. Kwa mujibu wa Beck (1999), vikatuni lazima viwe na ishara zake kwa sababu si kila kitu kinachowasilishwa ni ishara maalumu katika ufasiri wa maana ya paneli. Ishara ya msalaba iliongoza mfumo wa uelewaji wa maandishi kwenye mandhari ya paneli. Paneli hii ilieleweka kwa kuzingatia paneli zilizotangulia katika hadithi iliyosimuliwa.

Kwa mujibu wa Kraft (1978), katika Beck (1999), ishara muhimu katika vikatuni hueleza mandhari na matendo ya wahusika. Huendeleza msuko wa hadithi. Uchanganuzi makinifu wa diskosi hauangazii tu ujumbe unaowasilishwa kwa maandishi bali huchunguza vipengele vya kisimiotiki (Van Dijk, 1995), mfano msalaba katika mandhari ya paneli. Anavyosema Yus (2006), ni kuwa ufasiri wa ishara vikatunini hutegemea maarifa ya kiusuli ya msomaji. Hudokeza matarajio na machukulio ya kijamii kuhusu ulimwengu ambao ishara fulani zinapatikana. Ishara ya msalaba panelini ni ishara ya kisimiotiki iliyobainisha kuwa hema la vijana lipo mkabala na kanisa. Hema hili linatambuliwa kuwa sehemu ya ua la kanisa kutokana na ishara ya msalaba. Maneno ya mwandishi katika kielelezo cha 7:

Sunday afte (afternoon)
Jumapili adhuhuri

Nukuu hii ilithibitisha kuwa matukio panelini ni kwa mujibu wa siku ambayo mhusika JK alimrai Maria Kim ahudhurie mazoezi ya kwaya kanisani. Siku ya Jumapili iliipa paneli hii muwala wa jumla, aghalabu ni siku ya mapumziko. Vijana kupitia kwa paneli hii walishauriwa kutumia muda wao wa mapumziko kushiriki katika shughuli za kukuza vipaji. Mfano, kushiriki katika mazoezi ya kwaya ili kunoa vipaji vyao vya uimbaji.

Aidha, kifungu cha maneno: “Hema la Vijana” kilitambulisha wahusika kwenye hema kuwa ni vijana. Ina maana kuwa mazoezi ya kwaya yalifanyika katika hema la vijana ndani ya ua la kanisa. Paneli iliyofuata wahusika walionekana wakiwa na zana za muziki kama vile gitaa. Kulingana na paneli hii maandishi kwenye mandhari yalitambulisha mahali kwa kutaja mandhari panelini. Mahali palipotajwa palioana na msuko wa hadithi kwa kutambulisha wahusika ambao huenda hawaonekani panelini.

Hatimaye yalibainisha uhusiano uliopo baina ya michoro ya picha, yaani kanisa na hema la vijana katika mandhari ya paneli ili kuwa sehemu ya hadithi.

4.4.3 Hitimisho la Hadithi

Baadhi ya maneno ya mwandishi yalikuza muwala kwa kuashiria mwisho wa hadithi. Kwa mfano kifungu cha maneno katika kielelezo cha 8: *Mama Stacey Salon* kwenye ukuta wa chumba cha ususi:



Kielelezo cha 8, *Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 28

Kifungu cha maneno, “Mama Stacey Salon” kilichangia katika ujenzi wa msuko wa hadithi. Kilibainisha kuwa mhusika Nancy alienda kusuka nywele kwa “Mama Stacey Salon”. Nancy anaposema:

Haiya nyi wasee si tuchekiane
Wenzangu tukutane (Baadaye)
(Kielelezo cha 8, *Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 28)

Aliashiria kuwa hadithi hii imefika hatima. Hadithi iliwashirikisha wahusika watatu, Nancy alipoingia kwenye chumba cha ususi ni ishara kuwa wanafumukana. Msomaji hakutarajia kuendelea kwa hadithi baada ya kusoma kifungu, “Mama Stacey Salon.” Msomaji alipaswa kutumia mwonoulimwengu wake kujaza pengo la maarifa katika hadithi iliyosimuliwa. Kwa mujibu wa Nangira (2004), mwandishi si lazima aeleze kila kitu na ishara anazotumia. Maandishi kwenye ukuta yalimtoa mhusika Nancy hadithini na kumweka katika chumba cha ususi. Mahali ambapo hangeonekana wala kuwa sehemu ya hadithi tena. Pili, yalitoa kiini cha hadithi kufika hitimisho. Mhusika mmoja alipoingia katika chumba cha ususi wallobaki nje wanasambaratika. Hatimaye, yalitambulisha kuwepo kwa mhusika Mama Stacey panelini ingawa haonekani kwa

hadhira. Mlango uliowazi wa chumba cha ususi ni ishara kuwa mhusika Mama Stacey yumo chumbani. Ni machukulio ya mwandishi kuwa msomaji ana umilisi kuwa maandishi kwenye mandhari ya paneli, “Mama Stacey Salon” ndio mwisho wa hadithi.

4.4.4 Mabango ya Biashara

Mabango ya biashara hutekeleza wajibu wake kwa kujificha katika uhalisia wake na huashiria kitu ambacho kimefichama (Fairclough, 1989), ni vigumu vijana amba ni hadhira lengwa kuelewa athari zake. Baadhi ya kampuni zilizotangaza huduma zake katika *Shujaaz* ni zahanati za *T-safe* na *Safaricom*. Nembo za kampuni mbalimbali zilikuwa kwenye mabango panelini na zililenga kuwashawishi vijana kushabikia bidhaa au huduma zilizotangazwa. Nembo hizi ziliwabainishia vijana masuala yakuaminiwa kuhusu huduma au bidhaa. Imani iliyokuzwa huenda baadaye ikakita mizizi na kuwa itikadi (Van Dijk, 2001). Itikadi ambayo ingewaongoza vijana katika kutathmini kampuni wanazopendelea huduma au bidhaa zake (Wodak, 2008). Tazama kielelezo cha 9:



Kielelezo cha 9, *Shujaaz* chapta #3, ukurasa wa 7

Bango lenye istilahi “Safaricom” halina uhusiano na mada ya hadithi. Mandhari panelini ni mashambani kwa nyanya ya mhusika Malkia. Kwa mujibu wa Jigal (2006), aghalabu vikatuni vya Kiafrika hutangaza bidhaa katika mazingira na wahusika mashujaa amba ni wa Kiafrika. Ingawa, istilahi hii ilionekana kuwa na jukumu la kufahamisha kuhusu huduma za kampuni ya *Safaricom*, ilieneza mtazamo wa kiitikadi kama ilivyo katika diskosi za propaganda (Weiss & Wodak, 2003).

Safaricom ni kampuni ya kutoa huduma za mawasiliano nchini Kenya. Ulewaji wa paneli ulichangiwa na maarifa ya kiusuli walionayo vijana kuhusu ulimwengu wanamoishi. Nembo hii ilikuza muwala wa kijumla. Mandhari panelini ni nchini Kenya na yalikuza uhalisia hadithini. Uchanganuzi makinifu wa diskosi hutathmini michakato ya kijamii kutokana na kipindi mahususi cha kiwakati katika diskosi (Fairclough & Wodak, 1997). Nembo ya *Safaricom* iliiweka paneli hii katika kipindi maalumu cha kiwakati. Mabango ya biashara katika vikatuni yalikuza muwala kwa kuashiria eneo au hurejelea suala lenye msingi ya kihistoria. Hivyo basi matukio hadithini ni baada ya kuzinduliwa kwa kampuni hii. Ina maana kuwa diskosi ya *Shujaaz* ilisheheni maarifa na kumbukumbu za kijamii nchini Kenya.

Istilahi hii ilitangaza kusambaa kwa huduma za kampuni ya *Safaricom*. Dhana ya imani iliyokuzwa ni kutokana na ukweli kuwa kampuni hii hutamalaki taratibu za kuunda fikira na mawazo ya hadhira lengwa. Mchakato huu ulifanikisha kuundwa kwa hegemoni ya soko la kutoa huduma za mawasiliano ya simu ya rununu. Hatimaye, kuhalalisha ulimwengu ambao kampuni ya *Safaricom* ilihudumu bila ya kuwa na kampuni pinzani.

4.5 Maelezo ya Mwandishi.

Maelezo ya mwandishi huondoa utata wa maana panelini na huelekeza msomaji katika mchakato wa ufasiri wa maana (Badman, 2012). Kwa mujibu wa Saraceni (2000), maelezo ya mwandishi aghalabu hutoa habari za kumsaidia msomaji kukarabati mtiririko baina ya paneli ili kuziba pengo lililowasilishwa kwa gata. Maelezo ya mwandishi yametumiwa kukuza masuala yafuatayo hadithini:

4.5.1 Wakati

Kwa mujibu wa Yus (2006) wakati huwasilishwa kwa urahisi vikatunini kuitia kwa maelezo ya mwandishi. Neno au vifungu vya maneno kama vile “Baadaye” na “Siku iliyofuata asubuhi”, hudhihirisha wakati. Maneno ya mwandishi yalieleza kipindi cha wakati baina ya paneli mbalimbali katika hadithi (Mikkonen, 2017). Anavyosema Neil (2012), ni kuwa dhana ya wakati hukuzwa na yaliyomo panelini. Maelezo ya mwandishi yalieleza wakati usiodhahirika na unaodhahirika. Wakati usiodhahirika

ulibainika kwa matumizi ya vifungu vya maneno au neno kama vile “Baadaye: siku kadhaa”. Tazama Kielelezo cha 10:



Kielelezo cha 10, *Shujaaz* chapta #61, ukurasa wa 7

Baadaye: siku kadhaa

Baada ya siku kadhaa

Kifungu cha maneno, “Baadaye: siku kadhaa” katika paneli ya pili, kilidhihirisha kipindi cha wakati kisichobainika baina ya paneli ya kwanza na paneli ya pili. Kipindi ambacho ni kati ya siku mbili hadi siku sita. Ingechukua siku saba huenda kipindi hiki kingerejelewa kuwa, “Baada ya juma moja”. Kipindi hiki kilikuza muwala kwa kutaja makadirio ya muda kabla ya Poly na Knighty kuzungumza tena. Hii ni baada ya Knighty kumwambia Poly huenda amempachika mimba katika paneli iliyotangulia. Mazungumzo baina ya Poly na rafikiye ni kama ifuatavyo:

Rafiki wa Poly: Poly, Knight ako inje ya gate anadai kukuona.

Poly, Knight yupo nje ya lango (la shule) anaomba kukuona.

Poly: Sitachukua simu yake.

Sitapokea simu yake.

Jibu la Poly lilibainisha kuwa kifungu: “Baadaye: siku kadhaa” huenda ni kipindi ambacho alikuwa anajisahaulisha kuhusu Knight. Mhusika Knight kuwa mjamzito au la si tatizo kwake hadi pale alipoambiwa na rafiki yake kuwa alitafutwa na Knight. Ingawa, mapenzi walishiriki wawili, Knight ndiye huenda angetwikwa jukumu la kubeba ujauzito na kumlea mwana. Kwa mujibu wa Fairclough & Wodak (1997), diskosi husheheni itikadi. Vijana walishauriwa kujiepusha na mazoea ya kushiriki ngono bila kinga ili wasije wakajuta kama Knight kabla ya kugundua kuwa hakuwa

mjamzito. Hatimaye, kifungu hiki kiliweka nje matukio yaliyotokea baina ya paneli ya kwanza na paneli ya pili ambayo hayahusiana na mada wala msuko wa hadithi.

Aidha, maneno ya mwandishi hubainisha wakati maalumu. Tazama kielelezo cha 11:



Kielelezo cha 11, *Shujaaz* chapta #29, ukurasa wa 3)

Kwenye paneli kuna maelezo ya mwandishi:

*Monday Morning, 8:00.
Jumatatu saa mbili kamili za asubuhi.*

Kauli hii ilikuza muwala kwa kuwa kitangulizi cha hadithi. Matukio hadithini ni baada ya saa mbili kamili asubuhi. Kipindi “Jumatatu saa mbili asubuhi...” ni utangulizi wa hadithi. Kiliweka wazi utepetevu wa baadhi ya maafisa wa serikali wa kutofungua ofisi wakati uliofaa. Paneli iliyofuata mhusika Boyie alipata ofisi ya katibu wa kudumu haijafunguliwa. Matumizi ya kifungu “... Jumatatu saa mbili kamili za asubuhi...” kilikuza suala la kiitikadi. Itikadi iliyokuza muwala wa mantiki (Mullins, 1972). Msomaji alitarajia ofisi za serikali kuwa zimefunguliwa saa mbili kamili za asubuhi siku za juma. Maarifa ya kiusuli walijonayo vijana ni kuwa ofisi za serikali hufunguliwa wakati uliotajwa kwenye kifungu hiki nchini Kenya.

Kwa mujibu wa Van Dijk (1986), jukumu kuu la uchanganuzi makinifu wa diskosi ni kuchanganua wale walio mamlakani, wanaowajibikia suala fulani na wenye uwezo na fursa ya kuangazia changamoto za kijamii. Muwala ulikuzwa na kipindi hiki kwa kutambulisha sifa ya mhusika DJ Boyie kuwa mwenye kuwajibikia masuala ya vijana. Ni matarajio ya msomaji kuwa mhusika DJ Boyie kuwa mstari wa mbele katika kutafuta suluhu za changamoto zilizowakumba vijana. Matarajio ambayo yalitokana

na tajriba ya msomaji, mfumo wa imani uliokuzwa katika *Shujaaz*, mielekeo au maoni ya kibinafsi kuhusu mhusika huyu ambaye alikuwa na hadhi ya shujaa.

4.5.2 Siku ya Kutokea kwa Tukio

Baadhi ya maelezo ya mwandishi hutaja siku maalumu ya kutokea kwa tukio na hufafanua mandhari ya paneli. Maana ya kijumla ya paneli hujengwa kwa mandhari kuafikiana na matarajio ya hadhira kuhusu msuko wa hadithi (McCloud, 1993). Hii ni kwa sababu maana kamili ya paneli yalihalishwa na muktadha wa mandhari. Kwa mfano kielelezo cha 12:



Kielelezo cha 12, *Shujaaz* chapta #104, ukurasa wa 15

Paneli zilizotangulia wahusika wamekuwa wakijiandaa kwa siku ya michuano ya urembo. Msomaji anaposoma:

Siku ya auditions
Siku ya michuano


Msomaji anafahamu kuwa hii ni siku ambayo wahusika walikuwa wakijiandaa kushiriki na kubandika mabango yaliyoihusu. Mandhari katika kielelezo cha 12 yalifasiriwa kama ifuatayo: foleni ya watu ilitokana na idadi kubwa ya washiriki katika mashindano ya urembo. Ukumbi wa kijamii wa Jongo ulionekana ungechukua idadi kubwa ya hadhira na washiriki katika tamasha za urembo. Bango lenye picha ya mhusika wa jinsia ya kike katika ujirani wa ukumbi liliashiria kuwa washiriki si wa jinsia nyingine ila ya kike.

Majumba yaliyorundikana kwenye ujirani wa ukumbi ni ishara kuwa huu ni mtaa wa mabanda. Huenda ndio sababu wahusika wengi kuhudhuria michuano ya urembo.

Hatimaye, kwa mujibu wa Saraceni (2000), msuko wa paneli hubainika kuitia upana wa paneli. Paneli ndogo huashiria muda mfupi bali paneli pana aghalabu husheheni muda mrefu usiokatizwa. Ukubwa wa paneli hii ikilinganishwa na paneli nyingine hadithini uliashiria msuko mrefu, yaani tamasha hii ilichukua muda mrefu (Saraceni, 2000). Muktadha wa mandhari uliambatana na maarifa ya kiusuli ya vijana kuhusu michuano ya mashindano ya urembo na ulirahisisha uelewaji wa paneli.

4.5.3 Hitimisho la Hadithi

Maelezo ya mwandishi yalikuza muwala kwa kuashiria hitimisho la hadithi. Yalimwongoza msomaji “nje” ya hadithi ili baada ya kusoma asije akajiuliza “halafu?” (Wepler, 2011), mada katika utangulizi ikikosa kuangazia katika hadithi. Tazama kielelezo cha 13:



Kielelezo cha 13, *Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 21

And finally, ... My millions of fans.
Na mwisho... Mashabiki wangu mamilioni.

Nukuu hii ni ithibati kuwa shukrani kwa mashabiki ni kiini cha hadithi nzima.

Maneno ya mwandishi:

“... Na mwisho...”

Yana maana kuwa hakuna tukio jingine lingetukia baada ya kuangazia "... mashabiki wangu mamilioni...". Mhusika Boyie katika utangulizi aliwatabarukia mashabiki nakala ya #100. Mwandishi anaposema, "...mashabiki wangu milioni..." alitumia

mkakati wa takwimu. Kulingana na Van Dijk (1998), mkakati wa takwimu hutumiwa kushawishi na kusisitiza madai kwa kutumia nambari na takwimu. Takwimu zilizositisiza umaarufu wa jarida hili mionganoni mwa hadhira lengwa. Huu ni mkakati wa kuhakikisha kuwa kisa kuhusu mashabiki ni hitimisho la hadithi iliyokuwa inasimuliwa.

4.5.4 Usimulizi katika Nafsi ya Kwanza

Maelezo ya mwandishi huwasilishwa kuitia kwa usimulizi katika nafsi ya kwanza. Kwa mujibu wa Melnichuk (2013), mojawapo wa vipengele vinavyoendeleza muwala vikatunini ni masimulizi katika nafsi ya kwanza. Haya ni maelezo ya msimulizi yaliyotoa muhtasari wa matukio panelini na yalikuwa katika wakati uliopita. Ina maana kuwa matendo panelini ni katika mbinu rejeshi. Usimulizi wa aina hii ulifanikisha mpwito kutoka nafsi ya tatu ya usimulizi isiyokuwa ya mapendeleo ya kibinafsi hadi nafsi ya kwanza ambayo huwa nayo. Hatimaye uliendeleza msuko kwa kueleza hisia za kibinafsi za msimulizi. Tazama kielelezo cha 14:



Kielelezo cha 14, *Shujaaz* chapt #67, ukurasa wa 4

Mum alikuwa anajaribu kupigia simu na hampati, so akanipigia mimi kumtafuta...
Mama alikuwa anampigia simu (lakini) hapokei, kwa hivyo akanipigia (simu ili) nimtafute.

Nukuu hii ni masimulizi ya mhusika Albo kuhusu kilichoendelea panelini. Masimulizi ambayo yaliwasilishwa kama maneno ya mwandishi. Hata hivyo, alichosema hakiambatani na matendo yake. Kwa mujibu wa Saraceni (2000), maneno ya mwandishi wakati mwingine huwa na maana tofauti na paneli nzima. Yaliyomo huwa

hayaambatani na maana yaliyokuzwa na paneli nzima. Mtagusano baina ya maneno ya mwandishi na matukio huwa finyu au haupo. Hali hii ilikuza usambamba wa kimaana baina ya maneno ya mwandishi, mazungumzo na matendo ya mhusika Albo mtawalia. Kwa mfano, Albo anamwambia mama yake:

Sema mama aki si-watch Tv mum... nafanya revision.

Aisee! Mama kusema ukweli sitazami runinga...
ninadurusu.

Kauli hii ilikuza usambamba wa kimaana kati ya michoro ya picha na mazungumzo kati ya Albo na mama yake. Mazungumzo katika kielelezo cha 14 na matendo ya mhusika Albo hayakuzi dhana moja mahususi (McCloud, 1993). Maneno ya mwandishi yalihimiza suala la kutiliwa maanani: mhusika Albo kupigiwa simu na mama yake akitaka kujua aliko Faustina. Pia, ilibainisha sifa ya mhusika Albo kuwa mwongo. Alipotumia udanganyifu kushiriki ngono na Faustina baadaye msomaji alikubaliana na msuko wa tukio hili. Panelini Albo alimhadaa mama yake hatazami televisheni ilhali anaonekana akitazama (tazama kielelezo 14).

Mapendeleo ya kibinagsi katika paneli yalisawiriwa kupitia maneno ya mwandishi wala si kupitia matendo na usemi wa mhusika Albo kwenye paneli. Masimulizi yapo katika wakati uliopita ili kubainisha tofauti ya kiwakati baina ya matukio panelini na masimulizi ya wahusika. Msimulizi aliripoti kilichotendeka panelini. Pia, yaliwasilisha mapendeleo ya kibinagsi ya mhusika Albo kuhusu simu aliyopigwa. Kwa mfano, msimulizi anaposema:

“...akanipigia ili nimtafute...”

Mhusika Albo kama msimulizi alikuwa na uwezo wa kumpata Faustina, kwa sababu ye ye ni mwana wa mwajiri. Kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi mahusiano ya uwezo huzaliwa, hutumiwa na huzaana kupitia diskosi. Msomaji hawezi kuthibitisha iwapo kulikuwepo na mtu mwengine ambaye angetwikwa jukumu la kumtafuta Faustina au la. Maelezo ya mwandishi yalishinikiza msomaji kufuata mkondo mahususi wa matukio hadithini kulingana na mwonoulimwengu wa maandishi.

4.6 Uzungumzi Nafsi

Uzungumzi nafsi ni usemi ambao hauhitaji majibu (Crystal & Davy, 1969). Uzungumzi nafsi ulibainika kwa maandishi au michoro kuwa ndani ya mchoro wa umbo la mawingu na ulihusisha kauli na mhusika. Aidha, uliashiria fikira au mazungumzo ya mhusika katika vikatuni (Badman, 2012). Uzungumzi nafsi uliwasilishwa kwa mfumo wa michoro ya pitcha au maandishi katika data ya utafiti huu. Uzungumzi nafsi ulikuza muwala kwa kubainisha hisia au maoni ya kibinafsi ya mhusika. Ikumbukwe kuwa uzumgumzi nafsi katika vikatuni ni kwa manufaa ya msomaji katika kukuza msuko wa hadithi.

4.6.1 Uzungumzi Nafsi Uliowasilishwa kwa Michoro ya Picha

Michoro ya pitcha ilikuza muwala kwa kufafanua zaidi usemi wa mhusika. Kwa mfano, tazama kielelezo cha 15:



Kielelezo cha 15, *Shujaaaz* chapta #43, ukurasa wa 19

Paneli hizi zilirejelea madai kuhusu madhara mbalimbali (kama yapo) ya njia za kupanga uzazi. Paneli ya kwanza mhusika anasema:

*Mnatumia pills? Msitumie! Huwa zinajaa kwa tumbo halafu inafura
Mnatumia tembe (za kupanga uzazi)? Msitumie huwa zinajaa
tumboni halafu linafura.*

Mchoro wa picha uliofanua kauli hii ni wa mtu mzima wa jinsia ya kike aliyefura tumbo. Ikiwa picha hii ingekuwa ya mhusika mwanaume aliyena kitambi ingekosa mantiki. Paneli ilihusu njia za kupanga uzazi kwa wanawake.

Paneli ya pili, mhusika anasema:

Usitumie shindano. Huwa inafanya mtu azae watoi wanakaa kama mbuzi.

Usitumie sindano. Husababisha mtu (mwanamke) azae watoto wanaofanana na mbuzi.

Nukuu hii ilifasiriwa zaidi na picha ya mtoto mchanga mwenye pembe, ndevu na masikio kama ya beberu. Picha ya mtoto ilitazamisha taswira ya maelezo ya mhusika.

Hatimaye, paneli ya tatu mhusika anasema:

Mimi nilisikia ukitumia coil, huwa inasonga mpaka places zingine kwa mwili na inaweza cause injury.

Mimi nilisikia ukitumia chombo cha shaba huwa kinasonga hadi sehemu nyingine za mwili na kinaweza sababisha jeraha.

Nukuu hii ilifanuliwa zaidi na mchoro wa chombo cha shaba uliopo mwilini karibu na moyo. “Sehemu nyingine ya mwili...” ilipewa umahususi zaidi na chombo cha shaba kilichokaribia mchoro wa moyo. Kwa mujibu wa Jacobs (2007), uhushishaji wa mchoro ya picha na maandishi hufanikisha upataji wa maana ya maneno panelini. Chombo cha shaba kilichorejelewa panelini huenda kingesababisha jeraha rohoni au kifo ikiwa kingetumiwa kama mbinu ya upangaji uzazi. Picha katika paneli hizi ziliakuza muwala wa kijumla kwa kuwatazamisha vijana kuhusu imani potovu kuhusu mbinu mbalimbali za upangaji uzazi. Michoro iliyowasilishwa kama uzungumzi nafsi ilipambanua maana ya kauli za kila husika (Piro, 2002).

Mwandishi alitumia mamlaka yake katika kijamii kuwaelimisha vijana kuhusu imani potovu ya upangaji uzazi. Van Dijk (2001), anafafanua dhana mamlaka ya kijamii kuwa ni udhibiti wa kikundi chenye mamlaka katika kudhibiti matendo na akili ya vikundi vingine. Hali hii ilitokana na namna mwandishi alivyokejeli dhana potovu kuhusu upangaji wa uzazi wa kisasa. Vijana walizinduliwa na kushawishiwa kuhusu utumiaji mbinu hizi kwa kutolewa maarifa zaidi kuzihusu. Kwa mujibu wa Van Dijk

(2001), nguvu za ushawishi hutokana na maarifa, habari na mamlaka. Michoro hii ilitumika kuafikia malengo ya kuwaelimisha vijana kuhusu mbinu mbalimbali za upangaji uzazi.

4.6.2 Uzungumzi Nafsi Unaowasilishwa kwa maandishi

Uzungumzi nafsi uliowasilishwa kwa maandishi ulidhihirisha maoni ya mhusika kuhusu kinachotendeka panelini. Kwa mfano, kielelezo cha 16:



Kielelezo cha 16, *Shujaaz* chapta #29, ukurasa wa 3

Nimefika mapema hii meeting?
Nimefika mapema kwa mkutano huu?

Nukuu hii ilidhihirisha kuwa mhusika DJ Boyie hakupata ofisi ya katibu wa kudumu ikiwa imefunguliwa. Kwa mujibu wa Haque (2008), uchanganuzi makinifu wa diskosi husaidia katika uchanganuzi kuhusu masuala yaliyofiche ambayo ni changamoto katika jamii. Istilahi “Mapema” katika nukuu hii iliashiria kuwa DJ Boyie alifika kabla ya ofisi ya katibu wa kudumu kufunguliwa, licha ya kuwa wakati rasmi wa ofisi za kiserikali kufunguliwa. Iliangazia changamoto zilizowakumba vijana waliofafuta huduma za serikali. Kauli ya mhusika Boyie panelini ilikuza muwala kwa kuweka wazi mtazamo wa mwandishi kuhusu kuchelewa kufunguliwa kwa ofisi za serikali. Kwa mujibu wa Blommaert (2005), uchanganuzi makinifu wa diskosi ni kuchunguza athari za mamlaka katika diskosi iliyozalishwa katika matumizi ya jumla ya muktadha mahususi. Huenda mhusika DJ Boyie hakusema kwa sauti kwa kuhofia kuwa mhusika mwenzake aliye na mamlaka kumpiku angemsikia na huenda hangemhudumia.

4.7 Hitimisho

Lengo la sura hii lilikuwa kueleza namna muwala ulivyopatikana katika vikatuni vya *Shujaaz*. Muwala katika sampuli ya jarida hili ulikuzwa na: mada, sauti za kionomatopeya, maandishi katika mandhari ya paneli, maelezo ya mwandishi na uzungumzi nafsi na ulitokea katika viwango vitatu: mada, namna paneli zinavyohusiana kimaana ili kujenga msuko wa matukio katika diskosi na namna diskosi ilivyohusiana na maarifa ya kiusuli yaliyojenga muwala wa kijumla. Muwala wa kijumla ulikuwa mpana na ulihitaji muundo mkubwa. Muwala uliotokana na msuko wa matukio haukuwa umebainika barabara na haukuhitaji muundo mpana. Maandishi, ishara za kisimiotiki na michoro ya picha haifanyi kazi kivyake bali huhusiana ili kukuza muwala katika diskosi nzima ya vikatuni vya *Shujaaz*. Muwala wa jumla ulikuzwa kupitia mazoea ya kijamii ambayo yaliangaziwa katika sura ya tano.

SURA YA TANO

MIKAKATI YA MAZOEA YA KIJAMII KATIKA SHUJAAZ

5.1 Utangulizi

Mazoea ya kijamii ni namna kitu fulani kinavyowasilishwa katika diskosi. Kwa mujibu wa mchakato wa mazoea ya kijamii diskosi ni kitu ambacho huzaliwa, husambazwa na hutumika katika muktadha mahususi. Mchakato huu hurejelea sheria, miiko na hulka. Hutawala fikira, matendo na mahusiano katika jamii. Mikakati hii iliwasilishwa kupitia kwa mada zilizoteuliwa kiustadi katika diskosi ya *Shujaaz* ili kushawishi vijana kukubali mahusiano ya uwezo katika diskosi. Ni pamoja na: unominishaji, jazanda, ujumlishaji, utata wa maana na deiksisi nafsi.

5.2 Unominishaji

Unominishaji ni hali ya kutumia nomino badala ya vitenzi. “Kubadilisha vitenzi kuwa nomino” (Billig, 2008). Billig (ametajwa), anasema kuwa unominishaji hubadili mfumo wa kutenda. Istilahi ilio zao la mchakato unominishaji ilirejelea kuwepo kwa kitendo fulani au mfumo fulani. Mwandishi wa jarida la *Shujaaz* alitumia dhana za kidhahania kuwarejelea watekelezaji wa mifumo mbalimbali katika jamii. Unominishaji uliashiria mwelekeo wa mwandishi kuhusu mada fulani. Maarifa kuhusu unominishaji yalikuwa muhimu katika kuelewa maana ya diskosi nzima. Unominishaji ulibainika katika utafiti huu kupitia kwa istilahi:

5.2.1 Hustla

Istilahi *hustla* ni kutoka msimbo wa Sheng. “Hustla” katika umoja na “mahustlas” katika wingi na ilitokana na kitenzi “kuhustle”. *Hustla* katika muktadha wa diskosi ya *Shujaaz* ni wahusika waliojajiri kutokana na bidii yao licha ya kupitia changamoto chungu nzima. Wao walikuwa na mikakati mwafaka ya kubuni ajira na walivumbua mbinu za kuanzisha na kuendeleza biashara ili kujajiri binafsi. Baadaye hufanikiwa na alishiriki shughuli kama vile kuanzisha biashara, kilimo au shughuli nyingine ile halali.

Hadithi kuhusu *hustla* ilikuwa mada kuu. Maisha ya *hustla* yaliwasilishwa kwa njia ya bayografia na yaliangazia vipengele fulani vyatashi yake. Masimulizi haya yalibainisha namna vijana walivyojipusha na aushi ya ultima. Kimsingi *Hustla*

alishiriki katika shughuli za uimbaji, ukulima, uchoraji na usogora wa kupiga ngoma. Vijana ambao si “hustla” walilalamika kuhusu ukosefu wa kazi na walifahamika kama “kinyonyi”. “Kinyonyi” alizembea na hangejimudu kiuchumi na maisha yake kwenda tenge na kuishi kwa kuombaomba. “Mahustlas” walienziwa kama kielelezo cha kuigwa na vijana. Wao hujibidiisha kazini iliwasije wakadharauliwa, wakakemewa na hata kusutwa na jamii. Istilahi *hustla* iliwasilishwa kama maneno ya mwandishi. Tazama kielelezo cha 17:



Kielelezo cha 17, *Shujaaz* chapta #67, ukurasa wa 12

Katika kielelezo cha 17 aliyeojiwa na Malkia ni Peter aliyevalia tisheti yenyе maandishi “hustla.” Unominishaji wa kitensi kuhustle ultokana na shughuli alizofanya *hustla*. Alifanya nini? Alipanga nini? Na vijana walitarajia nini kumhusu? (Van Dijk, 1989). Yeye ni “hustla” kwa sababu: alifanya biashara ya kuuza matunda, mboga, chai na chapati. Alianzisha biashara hii kutokana na mpango wa kuwekeza akiba katika shirika la “Muranga Youth Sacco”. Shirika hili liliyapa mahojiano uhalisia kwa sababu “Muranga” ni sehemu katika Jamhuri ya Kenya. Huenda hadhira lengwa ilikuwa na ufahamu kuihusu. Hatimaye, aliyeojiwa ni mtu katika ulimwengu wa uhalisia ambaye si mhusika wa kubuni.

Kutokana na mipango kabambe ya kuendeleza biashara, hustla; alipata faida ya shilingi elfu tatu kila mwezi na alikuwa na wafanyakazi wanne. Mafanikio yake kwenye biashara yalimletea ujitambulishaji kuwa *hustla*. Hali hii iliinua hadhi yake miongoni mwa vijana na ndio kisababishi kikuu cha kuhojiwa na Malkia. Kuhojiwa kwake kulifahamisha ni kwa nini watu fulani wala si wengine ni *hustla*. Mkakati huu

ulikuza mahusiano ya uwezo yasiyo kuwa na usawa baina ya *hustla* na *kinyonyi*. Hustla alikuwa na hadhi ya juu kwa sababu ya kuwa na rasilimali zilizotokana na juhudhi zao. Vijana kupitia kwa istilahi *hustla* walishurutishwa kuwa mstari wa mbele katika kubuni nafasi za kazi katika jamii.

5.2.2 Wazito

Neno *mzito* au wingi wake *wazito* ni kutoka msimbo wa Sheng. Neno hili hurejelea kitendo cha “kuweka uzito”, yaani kusalimiana kwa kugonganisha ngumi. Watu “huwekeana uzito” wanapopongezana au mtu kumpongeza mwenzake. *Mzito* humaanisha mtu muhimu. Baadhi ya *wazito* ni pamoja na: mashabiki wa *Shujaaz* au viongozi wa kisiasa. *Wazito* huwa bingwa katika ulingo fulani kama vile: Ushabiki wa kusoma *Shujaaz* au kuwa kiongozi wa kisiasa. Istilahi hii huashiria cheo fulani katika muktadha wa msimbo wa Sheng, yaani ni sehemu ya usonde jamii (Levinson, 1983). Kwa mfano, tazama kielelezo cha 18:



Kielelezo cha 18, *Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 10

Keep it locked to Shujaaz na nitawaone tena in the next #100 chaptas wazito!

Endeleeni kusoma *Shujaaz* na nitawaona tena baada ya chapta #100 zitakazofuata, mashabiki!

Istilahi *wazito* ni unominishaji ulioegemea lengo. Ni kwa nini *wazito* walifanya walivyofanya? Mafanikio yao ni yapi? (Van Dijk, 1989). Hadhira lengwa ni “wazito” kwa sababu ya kusoma *Shujaaz*. Kutokana na mtindo wa usanii wa hali ya juu ya msimbo wa Sheng, *Shujaaz* ni maarufu sana mionganoni mwa vijana (Ngugi, 2017). Istilahi hii ilihalalisha usomaji wa jarida hili mionganoni mwa hadhira lengwa. Pia, ni mbinu mojawapo ya kudhibiti maarifa ya vijana kuhusu ni nani aliyepaswa kurejelewa kuwa “mzito.” Ushabiki ulichangia kuendelea kuchapishwa kwa jarida hili hadi kufikia nakala ya #100. Mkakati wa ujumlishaji ultumiwa kutambua mashabiki wote kuwa *wazito* (Fairclough, 2006). Mwandishi aliwaweka mashabiki katika kundi moja ili wajihisi kuwa sehemu ya kundi moja la *wazito*. Hata wale walioisoma nakala ya #100 kama nakala ya kwanza.

5.2.3 Fisi

Istilahi *fisi* katika umoja na *mafisi* katika wingi ni hali ya wahusika wanaume kuwa na tamaa ya kushiriki ngono. Ni mazoea ya kijamii kuwa aliyerejelewa kama *fisi* ana tamaa kama ya fisi mnyama. Diskosi ya *Shujaaz* kama diskosi nyingine yoyote ile husheheni utamaduni wa jamii (Wodak, 1997). Istilahi *fisi* huenda lilitokana na kitenzi *kufisia* chenye maana ya kutongoza wasichana wengi kwa dhamira ya kushiriki ngono nao. Vilevile *mafisi* ni vijana wavulana wazembe wasiokuwa na kazi na wao hutembea kwa makundi. Tazama, kielelezo cha 19:



Kielelezo cha 19, *Shujaaz* chapta #97, ukurasa wa 9

Panelini mhusika Maria Kim anawaambia wenzake:

Wah! Mafisi ndio hao.

Wah! (mshangao) Fisi ndio hao.

Istilahi *mafisi* inarejelea vijana wa jinsia ya kiume panelini. Mmoja wao anasema:

Gagaga! Mi napenda kale kako mbele.

Gagaga! (Mshangao) mimi ninampenda yule ametangulia.

Mhusika Chuxx anasema:

Mi napenda wote.

Mimi ninawapenda wote.

Kwa mujibu wa mhusika Maria Kim wahusika wavulana panelini ndio *mafisi*. Unominishaji katika muktadha huu ulijifunga kwenye imani ya kitamaduni ya jamii lugha, yaani fisi ni mnyama wa porini aliyeaminika kuwa na tamaa ya kupindukia. Hali hii iliibua maswali: Je, nini kibaya kumhusu fisi? Vijana hawakubaliwi kuiga sifa zipyi kutokana na *fisi*? (Van Dijk, 1989). Ute uliomtiririka mhusika Chuxx panelini ni dhihirisho la tamaa aliyonayo kwa “kuwapenda” wasichana wote. Ilibainisha kuwa wasichana ni waathiriwa wa matendo ya *mafisi* ya kuwa na hulka ya usherati. Paneli hii iliharamisha hulka za “*mafisi*” kwa kusitiza hulka hasi kuwahu. Uraibu wa *mafisi* ni kinyume cha maadili mema katika kijamii na ulipaswa kusutwa wala si kuigwa. Wao si waaminifu kwa wapenzi na hawajitolei mhanga kutafuta riziki. Hutumia muda mwingi katika pilkapilka za kuwatongoza wasichana.

5.2.4 Source

Istilahi *source* ilirejelea mhusika mwenye pesa. Istilahi hii ilihalalisha juhudzi za vijana kubuni ajira au kufanya kazi. Tazama kielelezo cha 20



Kielelezo cha 20, *Shujaaz* chapta #31, ukurasa wa 7

Leo nitawashika alafu nikue source.


Leo nitawachangamsha halafu niwe na hela.

Rasilimali ndio kichocheo cha kuwepo kwa istilahi *source*. Iliibua maswali, je, *source* alikuwa na nini ambacho wengine hawana? Hatimaye, rasilimali zipi zilizomilikiwa au zinazomilikiwa na *source*? (Van Dijk, 1989). Mhusika Man-like Kalito ana kipaji cha uimbaji. Huendeleza kipaji chake kwa kuwaburudisha wahusika katika hafla mbalimbali. Istilahi *source* panelini ni kipengele muhimu katika kueneza imani za itikadi ya kuwashawishi vijana kukumbatia bidii kama turathi muhimu maishani. Kwa mujibu wa Van Dijk (1995), itikadi hushirikisha vifaa vya kiakili kwa mfano mawazo, fikira, imani, maamuzi na turathi. Uchanganuzi makinifu wa diskosi uliangazia machukulio ya imani za kiitikadi yaliyofichika katika istilahi *source*. Yalilenga kuwafahamisha vijana umuhimu wa kubuni nafasi za ajira kwa kuendeleza vipaji vyao. Hivyo, watafanikiwa katika kijikimu maishani na kujiepusha na uhalifu.

5.2.5 Magava

Istilahi *magava* ni ya msimbo wa Sheng yenye maana sawa na neno ‘askari’ au “polisi”. Msingi wa istilahi hii ni kitenzi “kugavan”; yaani, kudhibiti watu kwa sababu ya kuwa na mamlaka fulani. Polisi huabiri gari lenye nambari za usajili “GK” wakielekea katika mitaa ya mabanda. Gari hili huenda ndio “ofisi” ya serikali iliyokaribu na vijana katika mitaa hii.

Mitaa ya mabanda aghalabu hukosa ofisi za serikali. Namna gari la polisi huwa limeandikwa kifupisho “GK”, yaani kwa urefu “Government of Kenya”, Serikali ya Kenya katika Kiswahili Sanifu. Wanaosafiri garini ni “magava”, yaani “serikali” kwa maana ya polisi. Wao huwasilisha maslahi ya serikali yaliyokuwa na uwezo za kudhibiti vijana dhidi ya kushiriki katika vitendo vya kiuhalifu. Tazama kielelezo cha 21 mshiriki Nancy Shanice alipochangia kuhusu masuala ya sheria, anasema:



Kielelezo cha 21, *Shujaaz* chapta #21, ukurasa wa 11

... *Tulikoboana na beste nguwarz nkamng'oa jino ju ya issue za chedaz. Jo nilindandiwa nama gva (magava) nilijipata kituo!* ...

... *Tulipigana na rafiki yangu nikamng'oa jino kwa sababu ya pesa. Nilitiwa mbaroni na polisi na kupelekwa (kwenye) kituo (cha polisi!)* ...

Uhusiano baina ya vijana na polisi ni msingi wa polisi kurejelewa kama *magava*. Je, uhusiano baina ya vijana wanaoishi katika mitaa ya mabanda na polisi ni upi? Je, polisi ni adui au wana mkabala mwema na vijana? (Van Dijk, 1989). Kwa mujibu wa Wodak (1997), kuundwa kwa diskosi ni suala kuu katika kinyang'anyiro cha mahusiano ya uwezo. Polisi wanamamlaka kuliko vijana kwa sababu wanawasilisha maslahi ya serikali. Huenda ndio sababu wanarejelewa na vijana kama *magava*.

Anavyosema Mesthrie (2000), ni kuwa lengo kuu la uchanganuzi makinifu wa diskosi katika uchanganuzi wa sampuli ya lugha ni kuweka wazi namna lugha, hudumisha au hurudufisha hali ya watu. Lugha hazitoshani na kulikuwa haja ya kutetea lugha za kundi la vijana. Istilahi *magava* iliyobainisha mahusiano ya uwezo yasiyokuwa na usawa na ilikuza mfumo wa unyanyasaji wa vijana. Kauli hii ilikuza imani za itikadi zisizo na sifa bia wala si zenye uwazi na utakatifu (Olowe, 1993). Wajibu wa istilahi katika kielelezo cha 21 ni kudhibiti fikira za vijana na kushinikiza itikadi ya wanaozalisha diskosi ya *Shujaaz* kuhusu polisi.

Kwa mujibu wa Fairclough (2002), diskosi haizalishwi bila muktadha na haiwezi kueleweka bila ya kuzingatia muktadha wa kipindi mahususi cha kihistoria. Kulingana na muktadha wa jamii uhusiano baina ya *magava* na vijana ni wa kiuhasama. Kwa mujibu wa Van Dijk (1998), nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi husaili mielekeo ya diskosi inayohusu matumizi ya nguvu, udhalimu na utabaka unaotokana na matumizi mabaya ya mamlaka. Uhasama huu ultokana na ukatili wa baadhi ya maafisa wa polisi.

Baadhi ya ukatili wanaoendelezwa na polisi katika *Shujaaz* ni pamoja na mauaji ya kiholela, kuwajeruhi, kutiwa mbaroni kwa vijana bila hatia na kuwasingizia mashtaka. Istilahi "magava" iliashiria nguvu za kihegemoni walizo nazo polisi dhidi ya vijana.

Huenda hakuna hatua za kisheria wangechukuliwa polisi kwa sababu ya sheria iliyowalinda. Wanapotumia nguvu kupita kiasi katika kudumisha amani na uzingatifu wa sheria. Kwa mujibu wa Rahimi & Riasati (2011), lugha hutekeleza wajibu wa kuangazia mabadiliko na uzalishaji wa itikadi. Istilahi hii ilitazamia kuwazindua wanajamii kupinga ukatili wa polisi katika mitaa ya mabanda nchini Kenya.

5.3 Jazanda

Tafiti kuhusu jazanda zilizowasilishwa kupitia kwa mazungumzo zilifuatiwa na tafiti kuhusu jazanda zilizowasilishwa kwa michoro ya “kutazamwa” (Forceville, 2009). Njogu & Chimerah (1999), wanasema kuwa jazanda ni mafumbo ambayo ndani mwake maana ya kitu imefichama. Forceville (2009), anapendekeza kuzingatiwa kwa ishara zifuatazo katika kuangazia jazanda zilizowasilishwa kwa michoro ya picha; picha na maandishi pamoja na: mazungumzo ya wahusika, viziada lugha, sauti, muziki, mnuso, mwonjo na mguso.

Tofauti na jazanda iliyowasilishwa kwa maandishi jazanda ya michoro ya picha huandikwa kwa “lugha ya kutazamwa”. Kulingana na Lakoff na John (1980) kwa ujumla jazanda hukuza fikira na kuibua maana ya dhana dhahania. Jazanda katika diskosi ya *Shujaaz* zilikuza: maoni, falsafa, matarajio, mielekeo, mitazamo, uelewaji na ufasiri wa masuala mbalimbali katika muktadha wa vijana nchini Kenya.

5.3.1 Wingu Jeusi

Kwa mujibu wa Kress & Van Leeuwen (2002) rangi hutekeleza wajibu wa kidiskosi katika masuala ya kitamaduni na kijamii. Aidha, rangi huzua maana mbalimbali katika tamaduni tofauti tofauti na hufafanua maana ya dhana (Mc Cloud, 1993). Matumizi ya Rangi nyeusi kijazanda katika data ya utafiti huu ilirejelea hali ya taharuki. Tazama kielelezo cha 22:



Kielelezo cha 22, *Shujaaz* chapta #51, ukurasa wa 5

Panelini hali ya taharuki na hatari ilimkabili mhusika Jorah. Baada yeye kumpachika mimba msichana wa Mzee Roberts. Mimba hii iliyolinganishwa na wingu jeusi panelini. Kwa mujibu wa Lakoff & Johnson (1980), kuwepo kwa jazanda ni kuelewa na kushuhudia aina moja ya kitu kwa niaba ya kitu kingine. Kutanda kwa wingu jeusi huashiria kunyea kwa mvua ya gharika katika jamii mbalimbabli. Mvua ambayo athari zake aghalabuni uharibifu wa mali au hata kufa maji kwa baadhi ya watu na mifugo. Huenda mhusika Jorah alihofia kuwa shughuli zake za kilimo zingefeli. Hela ambazo alikuwa ametengea kilimo zingetumika katika malezi ya mwana na kugharamia mahitaji ya kifamilia. Mvua iliyomnyea Jorah panelini ni ishara kuwa baadhi ya madhara yameanza kumkumba. Mfano, kugombezwa na Mzee Roberts katika paneli iliyotangulia. Mchoro wa wingu jeusi uliwaonya vijana dhidi ya kushiriki ngono bila ya kutumia kinga. Aidha, kumsawiri mhusika Jorah kama mwathiriwa wa hulka ya kushiriki ngono bila kutumia kinga.

5.3.2 Kitu kilichoshikwa Mkononi cha Rangi Nyekundu

“Kitu kilichoshikwa mkononi cha rangi nyekundu” kimetumika kama mkakati wa jazanda. Tazama kielelezo cha 23:



Kielelezo cha 23, *Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 26

Panelini kitu kilicho mkononi mwa mhusika wa kike Fena chenye rangi nyekundu kililinganishwa na chupi. Mchoro huu ni tasfida ili kuepuka kuchora vazi ambalo ni mwiko kuwekwa hadharani. Uuirejelea kitu ambacho ni cha aibu. Lengo la kutumia mchoro huu ni dhana ya chupi ikubalike kuliko jinsi ilivyo katika uhalisia wake na ulihifadhi maadili, imani au falsafa za jamii (Mugambi, 2007). Mchoro panelini ulibadilisha uhalisia ili kuibua hisia tofauti mionganoni mwa hadhira. Anavyosema Widdowson (2000), ni kuwa uchanganuzi makinifu wa diskosi ni ufichuzi wa itikadi fiche katika diskosi. Aidha, chochote ambacho kimeandikwa katika diskosi ya *Shujaaz* huegemea itikadi fulani iliyoshabikiwa na mwandishi na wadhamini (Fowler, 1991). Mwandishi alitumia mkakati huu kuwakejeli na kuwafedhehesha vijana wanaoshiriki ngono ovyyoxyo kwenye shamba la mahindi.

5.3.3 Mate Yanayodondoka

Mate yanayodondoka mhusika yalitumika kijazanda. Tazama kielelezo cha 24:



Kielelezo cha 24, *Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 29

Mate yanayomdondoka mhusika Chuxx (mhusika wa kwanza kushoto) katika paneli ya kwanza yalilinganishwa na tamaa ya kushiriki ngono. Hali hii ilitokana na mhusika huyu kuitazama miguu ya wahusika wasichana panelini. Ni matarajio ya mwandishi kuwa imani za msomaji zimejengwana miundo ya mazoea ya kijamii iliyodhibiti ufasiri wa maana (Van Dijk, 2001), ili kufasiri kudondokwa kwa mate kuwa tamaa. Huu ni mkakati wa uwakilishiwa nafsi-hasi ambao ulisisitiza masuala hasi kuhusu *wao*, yaani Chuxx na wenzake.

Mafisi wana tamaa ya kushiriki ngono na wasichana wengi. Urefu wa paneli ni dhihirisho kuwa mhusika Chuxx alitazama miguu ya wasichana kwa muda mrefu. Yaani paneli ina msuko mrefu. Paneli ya pili ilifafanua zaidi kilichomvutia Chuxx si kingine bali ni miguu ya wasichana walioketi mkabala naye. *Miguu* katika diskosi za Sheng huashiria wanawake au mwanamke anayetumiwa kimapenzi kisha kuachwa au sehemu ya siri ya mwanamke. Maana iliyokuzwa na paneli hizi ni kuwa Chuxx alivutiwa na wasichana. *Miguu* iliweka bayana nia ya mhusika Chuxx kutamani kushiriki ngono na wasichana katika kielelezo cha 24 halafu awaache. Hatimaye, ilibainisha kiini cha mhusika Chuxx kudondokwa na mate.

5.3.4 Michoro ya Vifungu vya Miraa

Michoro ya vifungu vya miraa ni ishara ya kijazanda iliyobainika katika data ya utafiti huu. Tazama kielelezo cha 25:



Kielelezo cha 25, *Shujaaz* chapta #88, ukurasa wa 19

Michoro ya vifungu vya miraa vyenye rangi ya kijani kibichi panelini iliwalishwa *base*. *Base* ni sehemu ambayo vijana hupiga gumzo, yaani ngome. Aidha, ni kitambulisho cha vijana walioketi kuwa wahuni na wazembe. Kwa mujibu wa Phillips & Jorgensen (2002), mchakato wa diskosi ni mfumo muhimu wa mchakato wa kijamii unaochangia kuundwa kwa utambulisho na uwasilishaji wake kuitia kwa mazoea ya kijamii. Michoro hii ni mfumo wa mchakato uliochangia kuundwa kwa utambulisho wa vijana walioketi.

Kwanza, vijana walioketi ni wazembe walimwajiri Man-like Kalito kubandika mabango huku wao wakipiga gumzo kwenye *base*. Pili, ni wahuni walikataa kumlipa Man-like Kalito baada ya kubandika mabango. Hatimaye, wenye kiburi kwa sababu Man-like Kalito anapowasimulia kuhusu alivyofanya kazi mhusika Scarface anamjibu kwa kiburi:

Man-like Kalito: *Scarface, mimi ndio ule mseee, nimeshamada na niliweka hadi past town.*

Scarface nimefanya kazi kwa bidii, nimemaliza na niliweka (mabango) hadi nikapita jijini.

Scarface: *So?!*
 Kwa hivyo?!

Mageuzi yaliyotarajiwa kuitia kwa paneli ni kuwa vijana wajihadhari na mazoea ya kujistarehesha kwenye *base*. Anavyosema Carvalho (2000), ni kuwa mwandishi

hutumia mazoea ya kijamii kuafikia athari fulani ya makusudi. Mwandishi ilikusudiwa kuwakanya vijana dhidi ya kujistarehesha katika *base* badala ya kubuni njia za ujasiria mali. Wasije baadaye wakajiunga na vikundi vya wahalifu.

5.3.5 Bahari

Bahari isiyokuwa na mwisho paneli iliashiria mawazo chungu nzima. Tazama kielelezo cha 26:



Kielelezo cha 26, *Shujaaz* chapta #104, ukurasa wa 3

Bahari inayotazamwa na mhusika Goda panelini ilinganishwa na mawazo kuhusu njia bora ya kupanga uzazi na mpenziwe. Kupata mimba ni kitendo kisichokubalika sana miongoni mwa vijana. Wengi wao huwa wanafunzi ambapo hali kama hii huweza kusababisha kutimuliwa shulenii au kutaabika kulea mwana kwa sababu ya kukosa uwezo wa kiuchumi (Mugambi, 2007). Mbinu ya chuku ilitumia kulinganisha mawazo ya Goda na bahari isiyokuwa na mwisho. Mawazo haya yaliwasilishwa kwa namna iliyoyafanya yaonekane kuwa suala kubwa kuliko jinsi yalivyo katika uhalisia wake. Mkakati huu ulilenga kuwazindua vijana kugundua uzito wa suala hili. Kulingana na Van Dijk (1998), chuku ni mkakati wa kuwashawishi watu kukubali madai fulani kwa kutilia chumvi ili kushinikiza itikadi fulani. Mkakati huu uliwasisitizia vijana umuhimu wa kuomba ushauri wanapopatwa na msongo wa mawazo kuhusu masuala ya kimapenzi. Majibu waliyopata vijana kuitia kwa diskosi ya *Shujaaz* yalisheheni maslahi ya mwandishi na wafadhili na yalidhibiti mielekeo yao kuhusu upangaji wa uzazi.

Wodak (2001), anasitiza kuwa uchanganuzi makinifu wa diskosi huangazia hasa uchanganuzi wa miundo fiche na miundo wazi ya lugha katika kudhihirisha maamuzi na kudhibitiwa kwa jamii ambako huwekwa wazi kupitia kwa lugha. Kulingana na mtazamo huu uchanganuzi makinifu wa diskosi huangazia uhusiano uliopo baina ya lugha na mamlaka na kuitazama lugha kama mfumo wa muundo wa jamii. Mfumo huu unaweza kutumiwa vibaya na wadhamini na mwandishi katika kulazimisha au kuwasilisha imani za kiitikadi katika ushauri wao kwa vijana. Vijana walishauriwa kuomba nasaha kutoka kwa mashabiki wenzao au wataalamu wa afya ya uzazi. Huenda mitazamo ya washauri ikaendeleza maslahi ya wadhamini na mwandishi.

5.4 Ujumlishaji

Van Dijk (1998), anasema kuwa ujumlishaji ni uwasilishaji wa wanajamii katika makundi hasa katika hali hasi. Mkakati huu hufafanua mielekeo na itikadi ya makundi mengine kwa madai yaliyoyaharibia sifa. Ujumlishaji uliwaainisha wahusika katika makundi mbalimbali katika diskosi ya *Shujaaz*. Tazama kielelezo cha 27:



Kielelezo cha 27, *Shujaaz* chapta #21, ukurasa wa 4

UTINGO: *Eh, sibebangi viwete, hawalipangi gari! Dere twende.*
Eh (mshangao), gari huwa halibebi viwete (kwa sababu) huwa
 hawalipi nauli! Dereva endesha gari.

Maria Kim: *Ai?! Huyu si kiwete, ni mlemavu unaongeaje?!*
 Ai?! (mshangao) Huyu si kiwete, ni mlemavu unazumgumza
 (hivyo kwa nini?).

Kauli ya utingo iliweka wazi sifa hasi ya walemvu kama wasiokuwa na uwezo wa kiuchumi. Kwa mujibu wa Van Dijk (2006), ujumlishaji ni tukio ambapo mzungumzaji hujumlisha masuala kwa kutumia mifano mahususi katika kundi la *sisi*.

Japo kuna mlemavu mmoja, utingo alimrejelea kuwa, “viwete” katika hali ya wingi badala ya “kiwete” katika hali ya umoja. Maana ya kimsingi ya leksimu “kiwete” ni mtu aliyelemaa miguu. Hatembe. Istilahi “viwete” ina maana ya ulemavu kwa jumla katika muktadha wa paneli hii. Maana ya ziada ilijikita katika muktadha wa paneli. Masuala yafuatayo yaliibuka:

- i. Mlemavu wa aina yoyote ile ni kiwete.
- ii. Viwete (walemavu) wote huwa hawalipi nauli wanaposafiri kwa matatu.
- iii. Walemavu ni maskini kutokana na hali yao ya kuwa na ulemavu.

Ujumlishaji huu ulipotosha kwa sababu kuna walemavu wenyewe uwezo wa kiuchumi. Hadithi hii ilipiga jeki ujitalbulishaji wa kundi la vijana walemavu. Iliangazia changamoto zilizowakumba walemavu katika jamii. Hadithi yenye paneli thelathini, ishirini na nane zilielezea changamoto zilizowakumba walemavu. Huu ni mkakati wa mwandishi wa kuwatenga wanaowanyanya walemavu na kuwachukulia walemavu kuwa tofauti kutokana na hali maalumu iliyowakumba (Palfreyman 2002). Suala hili linashadidiwa na Van Dijk (2006), anaposema kuwa mwandishi kuitia kwa diskosi hugawa wahusika kwenye makundi yanayowasilisha maslahi ya *sisi* dhidi *wao*. Isitoshe, kusawiri kundi analounga mkono kuwa waathiriwa wa matendo ya *wao*. Mhusika utingo hakupewa nafasi kufafanua ni kwa nini gari halibebi walemavu. Paneli mbili tu zilitumika kumwangazia utingo.

5.5 Utata wa Maana

Kempson (1977), anaeleza kuwa utata wa maana ni hali ya kuwa na fasiri zaidi ya moja katika usemi. Uwazi katika maana ni kipimo cha umilisi wa mawasiliano ikiwa lengo la mawasiliano ni kupata maana isiyokuwa na utata (Eisenberg, 1984). Utata sentensi ni hali ambapo sentensi moja huwa na maana zaidi ya moja au huweza kueleweka kwa namna zaidi ya moja. Data ya utafiti huu ilidhihirisha kuwa baadhi ya sentensi zilikuwa na maana tata kwa sababu ya kutopeana habari za kutosha au kutoangazia dhana mahususi (Van Dijk, 2004).

Hata hivyo, ilibainisha kuwa utata wa maana ultokea kimakusudi. Mkakati huu ulimpa mwandishi mwanya wa kuepuka kutaja hadharani dhana zilizo miiko. Anavyosema Fairclough (1989), ni kuwa utata wa maana hutokeea katika sentensi

zenye maana tata ili matumizi yake yanapopingwa kwa vyovyote vile mwandishi hukwepa lawama kutokana na fasiri za msomaji. Hali hii ilimpa mwandishi nafasi ya kutowajibikia maana iliyofasiriwa. Utata wa maana ulitokea katika viwango viwili: kileksia na kimuundo.

5.5.1 Utata wa Kileksia

Huu ni utata unaosababishwa na istilahi fulani kwenye sentensi yenye maana zaidi ya moja (Saleh, 2018). Kwa mfano istilahi “ball” na “CD” katika data ya utafiti huu.

Mfano wa 1:

Istilahi *ball* ni ya msimbo wa Sheng iliyokopwa kutoka lugha ya Kiingereza yenye maana sawa na istilahi mpira kwa Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa Mugambi (2007), neno *ball* hutumiwa kurejelea kifaa cha duara kilichotengenezwa na ngozi na ambacho hutumika wakati wa michezo. Hata hivyo, istilahi *ball* katika muktadha wa msimbo huu ina maana ya: mpira wa kandanda, hali ya kucheza mpira wa kandanda na ujauzito. Istilahi hii ilipata upanuzi wa maana kisemantiki katika msimbo wa Sheng (Ogechi, 2005). Data ya utafiti huu ilidhihirisha aina mbili ya maana ya leksimu *ball*: ujauzito na mpira wa kandanda. Neno hili linatumika kuelezea lile umbo la duara la tumbo ya mjamzito na likikuwa na adabu zaidi ya neno lenyewe katika lugha ya kawaida (Mugambi, 2007). Utata katika kiwango hiki ultokana na neno *ball* kuwa na fahiwa zaidi ya moja kama ilivyodhihirika panelini. Tazama kielelezo cha 28:



Kielelezo cha 28, *Shujaaaz* chapta #41, ukurasa wa 21

Betty: *Wewe Chuxx ulinipa ball! Ulifanya niache shule sasa sina dooh.*

Wewe (Chuxx) ulinipa mpira (ball)! uliosababisha niwacheshule sasa sina pesa.

Chuxx: *Na tutajuaje huyo mtoi ni wangu?*

Na tutajuaje mtoto huyo ni wangu?

Kifungu “... ulinipa ball...” katika kielelezo cha 28 kina maana ya: alipatiwa mpira wa kandanda au alipachikwa mimba. Kwanza, mhusika Chuxx alimkabidhi mhusika Betty mpira wa kandanda uliosababisha yeze kukosa kwenda shule na kukosa kuwa na pesa. Pili, kilikuwa na maana ya alimpa uja uzito. Hali hii ni kwa sababu:

- i. Mzungumzaji ni mhusika kijana wa jinsia ya kike na anaweza kupata ujauzito.
- ii. Anayeambiwa ni mhusika wa kiume na anaweza kumpachika mimba msemaji.
- iii. Anayeambiwa anajibu kuwa alishuku ikiwa mtoto ni alikuwa wake.

Hata hivyo, istilahi *mtoi* katika msimbo wa Sheng aghalabu ina maana ya msichana mrembo. Huenda *mtoi* aliyerejelewa na Chuxx kisiwe kijusi tumboni mwa Betty. Kwa mujibu wa Einsenberg (1984), kuna miktadha mbalimbali ambayo utata wa maana huwa na manufaa kuliko mawasiliano yasiyokuwa na utata. Maana iliyofasiriwa ni ujauzito. Baadhi ya msamati wa msimbo wa Sheng huzingatia mbinu ya tasfida (Kobia & Kinge'i, 2007). Leiksimu *ball* imetumika kitasfida ili kuepuka kutaja neno mimba ambalo ni mwiko kutajwa hadharani na ilipunguza ukali wa neno “mimba” na kuhifadhi adabu ya lugha na kukwepa kujadili hadharani masuala ya unyumba.

Mfano wa 2:

Istilahi *CD* ni ufupisho wa maneno mawili ya lugha ya Kiingereza *condom* (kondomu) au *compact disk* (santuri). *CD* ni dokezo la maneno kamili (Kobia & Kinge'i, 2007). Ingawa, istilahi *CD* zinaelekea kuwa na matamshi na tahajia zinazofanana zina vyanzo tofauti. Kwa mujibu wa Temu (1990), hii ni mbinu ya uleksikalishaji inayohusu ufupishaji wa istilahi kwa mintarafu ya kuunda leksimu mpya. Herufi au silabi za mwanzo wa maneno yanayofupishwa huunganishwa ili kujenga umbo jipya linalobeba maana. Mbinu hii huwa haitumiwi mara nyingi katika uundaji wa istilahi (Obuchi & Mukhwana, 2010). Tazama mfano katika kielelezo cha 29:



Kielelezo cha 29, *Shujaaz* chupta #59, ukurasa wa 22

Mhusika A: *Cheki huu kuro, kazi ni kubebe CD kwa bag.*

Tazama huyu kahaba, kazi yake ni kubebe CD kwa mkoba.

Mhusika B: *Ni dem wa aina gani hu-do hivo?*

Ni msichana wa aina gani hufanya hivyo?

Mhusika Pam: *Huh! Hawa madem wana nisema nini?*

Huh! (mshangao) wasichana hawa wanansengenya kwa nini?

Kauli ya mhusika “A” ina maana tata na ilifasiriwa kwa namna mbili:

- i. Mhusika Pam ni kahaba kwa sababu alikuwa na mazoea ya kubebe santuri kwenye mkoba.
- ii. Mhusika Pam ni kahaba kwa sababu anamazoea ya kubebe kondomu kwenye mkoba.

Maana hizi zinatokana na mantiki kuwa santuri na kondomu zote zingetoshea kwenye mkoba wa Pam. Uhusiano wa maana hii ni kutokana na neno *CD* kuwa na maana zisizohusiana kihistoria (Crystal, 1987). Maana iliyokusudiwa kwa kuzingatia muktadha panelini ni maana ya (ii). Maana haya ni mwiko kujadiliwa hadharani katika jamii. Kwa mujibu wa Mugambi (2007), matumizi ya lugha mwiko yamefungiwa kwa kigezo mahususi vya kitamaduni. Neno huwa mwiko kama linaibua hisia kwa msikilizaji, linakufuru au kuvuruga imani ya wanajamii. Aidha, hukiuka adabu kama ni chafu, baya, husababisha hisia mbaya. Maana ya (i) si mwiko na imezoleka. Utata huu ulikusudia kufanikisha lengo la kujadili dhana ya kondomu hadharani bila ya hatari ya kupotoka kimaadili (Leitch & Davenport, 2007).

5.5.2 Utata wa Kimuundo

Utata wa kimuundo hutokana na namna sentensi ilivyopangiliwa kwa kurejelea umbo; kirai au neno kuwa katika nafasi maalumu sentensini (Saleh, 2018).

Mfano wa 1,

Tazama kielelezo cha 30:



Kielelezo cha 30, *Shujaaz* chapta #51, ukurasa wa 19

Mhusika A: *Kaone kamekuja kutunyang'anya job.*

Mwone huyu amekuja kunyakua kazi.

Mhusika B: *Nafikiri ndio kalifanya Nancy akafutwa.*

Ninadhani yeye ndiye alisababisha Nancy afutwe kazi.

Mhusika CH: *Kanakaa kanapeana rahisi.*

Anaonekana kupeana rahisi.

Kifungu cha maneno, “Anaonekana kupeana rahisi” kilichohusishwa na mhusika “CH”, hakitoi habari za kutosha ili kieleweke. Hakijakamilika (Hutchby, 2001). Hali hii inaibua suala kuwa kilichopeanwa hakijatajwa na Lengo la mwandishi kutumia halijabainika barabara. Mhusika kumrejelea Maria Kim kwa kiambishi cha nafsi “ka” kulidunisha hadhi yake kwa sababu si mmoja wao. Ni mkakati wa kuendeleza sifa hasi kuhusu Maria Kim ambaye si *sisi* (Van Dijk, 2006). Hali hii inafafanuliwa zaidi na Van Dijk (1997), anaposema kuwa mawasiliano yenyе utata husheheni maana mbalimbali ambayo washiriki katika mawasiliano huafikia malengo yao. Kinachopeanwa hakijatajwa. Kitende “kupeana” kilipata mabadiliko yafahiwa ya ziada bila ya kupoteza maana asili katika Kiswahili Sanifu. Istilah *kupeana* ilipata upanuzi wa maana ili itumike katika miktadha mingi zaidi kuliko hapo awali katika msimbo wa Sheng (Lyons, 1981).

Kwa mujibu wa Mugambi (2007), upanuzi wa maana unahakikisha kuwa dhana zilizopo katika lugha zimetumiwa kwa ukamilifu au pana zaidi badala ya haja ya kubuni msamiati mpya kila mara. Leksimu –*peana* ina maana ya “kukabidhi”. Hata hivyo, panelini kitenzi –*peana* kina maana ya “hali ya mwanamke kukubali kushiriki ngono.” Ikizingatiwa kuwa anayeambiwa ni mhusika wa jinsia ya kike. Kitenzi hiki kina sifa za upolisemia na kilirejelea zaidi ya dhana moja panelini (Ogechi, 2005).

Tazama mfano wa 2

Tazama kielelezo cha 31:



Kielelezo cha 31, *Shujaaz* chapta #4, ukurasa wa 20

Lakini mrembo kama wewe *ongea vizuri* nikulipie.

Kifungu cha maneno, “ongea vizuri” kilikuza utata wa maana katika sentensi. Kiliibua swali, je, Maria Kim alipaswa kuongea vipi? Maana iliyofasiriwa ni kuwa mhusika Maria Kim ni mrembo lakini huenda hawezi kutamka maneno vizuri au kuzungumza kwa sauti inayosikika. Maana nyingine yaliyobainika ni kuwa “ukikubali kuwa na uhusiano wa kimapenzi.” Haya ndiyo maana ya dharura yaliyopatikana kuititia kwa jibu la Maria Kim:

Yaani huna hata aibu!
Yaani, hata hauna aibu!
(*Shujaaz* chapta #4, ukurasa wa 20)

Jibu hili lilishadidia kuwa maana yaliyokusudiwa ni: Mhusika diwani alivutiwa na urembo wa mhusika Maria Kim na alimpendekezea wawe na uhusiano wa kimapenzi ili amlipie karo. Maana haya yaliwekewa msingi na kitendo cha mhusika Diwani katika paneli ya kwanza kumkonyezea jicho la kulia Maria Kim. Paneli hizi zilidhamiria kuweka wazi masaibu yaliyowakumba vijana wa jinsia ya kike

wanapoenda ofisi za serikali kutafuta huduma mbalimbali. Hata hivyo, mhusika Maria Kim alikataa nia ya Diwani na huu ndio mwelekeo aliopendekeza mwandishi.

5.6 Deiksisi Nafsi

Deiksisi hurejelea uhusiano baina ya muundo wa lugha na miktadha ya matumizi (Levinson, 1983). Kwa mujibu wa Grundy (2000), deiksisi ni neno linalorejelea kuashiria au kuonyesha. Deiksisi nafsi hubainisha tofauti baina ya mzungumzaji, anayezungumziwa na mtu ye yote yule (Trask, 1999). Kwa mujibu wa Odebunmi and Olaniyan (2005) wanasema kuwa katika miktadha mbalimbali ya matumizi, kiwakilishi cha nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu hujumuisha: mzungumzaji, wanaozungumziwa na hutenga mzungumzaji na anayezungumziwa mtawalia. Hutambulisha ni nani anayezungumza (Crystal, 1985). Data ya utafiti huu ilishamiri matumizi ya deiksisi za nafsi zilizobainisha maslahi ya *sisi* dhidi ya *wao*. Zilitumiwa kujenga uhusiano, kukuza hisia za kuwa katika muungano au kuwatenga washiriki katika kundi fulani.

5.6.1 Deiksisi Nafsi ya Kwanza

Data ya utafiti huu ilidhihirisha kuwa na deiksisi ya nafsi ya kwanza wingi. Deiksisi *sisi* ili wajibika katika kuwaunganisha pamoja au kuwatenganisha wahusika. Ilileta umoja katika makundi mbalimbali. Ili potumiwa kutenga: ilitumika kugawa majukumu, ili chochote kinachojadiliwa na michakato ya sera iliyotekelizwa hakishurutishiwi mtu binafsi ila kundi nzima la watu (Van Dijk, 2002). Tazama kielelezo cha 32:




Kielelezo cha 32, *Shujaaz* chapta #43, ukurasa wa 7

Sisi kama mastude tulikatsika sana. Tukaamua kuambia class teacher lakini hakudo anything hata baada ya mwezi mmoja.
Sisi kama wanafunzi tuliudhika sana. Tukaamua kupiga ripoti kwa mwalimu wa darasa, lakini hakuchukua hatua yoyote hata baada ya mwezi mmoja.

Deiksisi *Sisi* iliwasilisha maslahi ya wanafunzi hadithini. Ilihalalisha uamuzi wa wanafunzi kuripoti walimu wanaokosa kuhudhuria vipindi vyta masomo. Pia, ilisambaza mzigo wa uwajibikaji na hofu ya kufasiriwa ipasavyo (Wilson, 1990). Mwanafunzi aliyeojiwa na Boyie panelini kwa ujasiri alijitwika jukumu la kuzungumza kwa niaba ya wanafunzi ambao ni *sisi* ili kuleta umoja mionganoni mwao. Anasawiri *sisi* kama wenye bidii ya kwenda shulen, waadilifu, waliheshimu mkondo wa mawasiliano katika muktadha rasmi wa shulen. Walianza na mwalimu wa darasa hadi kwa naibu wa mwalimu mkuu. *Sisi* ni waathiriwa wa mazoea ya walimu kukosa kuhudhuria vipindi vyta masomo shulen. Hatimaye, iliashiria kuwa msemaji na msomaji walikuwa katika kundi moja.

5.6.2 Deiksisi Nafsi ya Pili

Data ya utafiti huu ilikuwa na deiksisi za nafsi ya pili *wewe* katika hali ya umoja na *nyinyi* katika hali ya wingi mtawalia. Utafiti huu uliangazia mfano mmoja kwa kila hali zote za deiksisi ya nafsi ya pili. Mfano katika paneli (kielelezo cha 33) kauli ya mhusika Mama Stacey ilidhihirisha matumizi ya deiksisi nafsi ya pili umoja, *wewe*.



Kielelezo cha 33, *Shujaaz* chapta #39, ukurasa wa 20

Mama Stacey: Na ujue wewe ndiye unalipia bill za Betty hosi.

Ujue wewe ndiye unamlipia Betty gharama za matibabu hospitalini.

Deikisisi *wewe* iliwakilisha mhusika Chuxx ambaye hawasilishi maslahi ya *sisi*. *Sisi* ni akina Mama Stacey na wenzake panelini. Deikisisi *wewe* ilidhihirisha tofauti za kitiikadi baina ya Mama Stacey na Chuxx. Mhusika Chuxx alimpachika mimba Betty kisha alimpa dawa ya kuavya mimba. Betty alipopelekwa hospitalini baada ya kumeza tembe za kuavya mimba, Chuxx alibaki akijivinjari kwa vileo. Kulingana na Kuo (2002), deikisisi *wewe* hutumiwa kukuza umoja au kushambulia wapinzani. *Wewe* ilimshambulia moja kwa moja mhusika Chuxx kwa sababu ya kumpa Betty tembe za kuavya mimba. Aidha, ilikuza umoja baina ya Mama Stacey na wenzake na kumshutumu mhusika Chuxx kwa kumpa Betty tembe za kuavya mimba.

Aidha, hali kama hii ilitokea katika wingi wa deikisisi nafsi ya pili wingi, *nyinyi*.

Tazama kielelezo cha 34:



Kielelezo cha 34, *Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 26

Mzee Jared: Nyinyi watoto! Tabia mbaya! Hii kijana ndio inaharibu wasichana wetu! Nyinyi ndio mnafanya hii mahindi inakulwa nawadudu!

Nyinyi watoto (mna) tabia mbaya, huyu kijana anaharibu wasichana wetu! Nyinyi ndio mnafanya mahindi haya yanaharibiwana wadudu!

Deikisisi *nyinyi* ilidhihirisha udhaifu wa Fena na Denis wa kukishiriki ngono katika shamba la mahindi. Anavyosema Austin (1962), ni kuwa *nyinyi* hutumiwa na mtu au kundi la watu kudhihirisha mamlaka. Ilitenga mhusika Mzee Jared na wahusika Fena na Albo. Kwa azma ya kuwalaumu Albo na Fena kwa kushiriki ngono kiholela bila kutumia kinga na mhusika Mzee Jared hataki kujihuisha nao na aliwasilisha maslahi ya baadhi ya wanajamii ambao walikuwa tayari kuwarekebisha vijana walioshiriki ngono kiholela bila ya kutumia kinga. Aidha, ilisisitiza kuzoroteka kwa madili ya wahusika wanaofumaniwa wakishiriki ngono. Pia, ilimsawiri kama Mzee Jared kigezo cha kutathmini uhalali wa michakato ya jamii. Hatimaye, alihalalisha kitendo cha kuwafumania na kuwacharaza Fena na Denis wakishiriki ngono kwenye mahindi katika paneli iliyotangulia.

5.6.3 Deikisisi Nafsi ya Tatu

Deikisisi za nafsi ya tatu humrejelea mtu ambaye si msemaji katika tukio la mawasiliano. Anaweza kuwa mrejelewa au hadhira isiyokuwa msemewa (Levinson, 1983). Deikisisi ya nafsi ya tatu ni *yeye* na *wao* katika hali ya umoja na wingi mtawalia. Matumizi ya deikisisi ya nafsi ya tatu wingi, *wao* yalibainika katika data ya utafiti huu. Paneli (kielelezo cha 35) ifuatayo mhusika anasema:



Kielelezo cha 35, *Shujaaz* chapta #3, ukurasa wa 6

*Wao waligive up lakini sisi tulitia bidii ... Sasa dooh zimetoka,
tunaanza kuexpand bizna.*

Wao walikata tamaa lakini sisi tulitia bidii ... Sasa pesa za mkopo
zimetoka tunaanza kupanua biashara.

Deiksisi *wao* iliwasilisha sifa hasi za vijana wenye mazoea ya kurandaranda katika mitaa ya mabanda. Huu ni mkakati wa mazoea ya kijamii uliobainisha uhasama baina ya kundi la *sisi* dhidi ya *wao*. Kwa mujibu wa Van Dijk (1998), mkakati wa uhasama hutenga maslahi ya *sisi* wenye sifa chanya na *wao* wenye sifa hasi. Mzungumzaji alisawiri sifa hasi za *wao* amba si wanachama wa kundi lao. *Wao* hawajui namna ya kujaza fomu za kuomba mkopo kutoka kwa Hazina ya Vijana wala kuandika pendekezo la mradi wa biashara. Hatimaye ni wazembe katika kutimiza mahitaji ya kujaza fomu za kuomba mkopo na hawana umoja katika kikundi chao.

Sisi ni vijana walioanzisha biashara ya kuuza vyakula. Mmoja wao alimpigia simu DJ B kumjulisha kuhusu mafanikio yao kwenye biashara ya kuchuuza chakula. Baada ya kuomba mkopo, biashara ilipanuka na walisambaza vyakula kwa shule na vyuo vya anuwai. Huu ni mkakati wa kusisitiza sifa chanya za *sisi* kama kundi kielelezo huku akisisitiza masuala hasi kuhusu *wao* kama kundi linalopaswa kupuuzwa kukejeliwa na kuchekwa (Van Dijk, 2006). Hatimaye, *wao* walisawiriwa kama adui wa msemaji na msomaji na kuwaweka katika kikundi kimoja.

5.7 Hitimisho

Sura hii ilifafanua mikakati ya mazoea ya kijamii katika *Shujaaz*. Ilibainika kuwa *Shujaaz* huwasilishwa kwa unominishaji, jazanda, ujumlishaji, utata wa maana na deiksisi nafsi. Mikakati hii ilisheheni mada ambazo ziliteuliwa kwa ustadi ili kushawishi hadhira kukubali mamlaka yaliyomo katika diskosi na kujenga matumaini kuhusu maisha ya baadaye. Iliwashawishi vijana kutambua, kuendeleza na kushabikia mada zinazoangaziwa katika *Shujaaz*. Mazoea ya kijamii yaliendeleza mahusiano mbalimbali ya uwezo yaliloangaziwa katika sura ya sita.

SURA YA SITA

MAHUSIANO YA UWEZO KATIKA SHUJAAZ

6.1 Utangulizi

Uchanganuzi makinifu wa diskosi huchunguza namna mahusiano ya uwezo hujengwa kuitia kwa lugha. Uwezo ni watu kumtii mwengine kwa hiari bila ya kushurutishwa. Watu wenge hadhi ya juu kuliko wengine katika makundi mbalimbali ya kijamii hutumia lugha kama dhihirisho la uwezo wao. Lugha hudhibiti namna watu hutagusana kulingana na uwezo. Data ya utafiti huu ilidhihirisha kuwa kuna mahusiano ya uwezo baina ya makundi mbalimbali katika diskosi ya *Shujaaz*.

6.2 Wahusika

Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa kuna mahusiano ya uwezo baina ya wahusika mashujaa na wahusika wa kawaida. Kutambulika kwa mhusika ni sifa ya kimsingi ya vikatuni (Mikkonen, 2017). Wahusika mashujaa katika jarida la *Shujaaz* ni pamoja na: DJ Boyie, Charlie Pele, Malkia na Maria Kim. Mfano, katika (*Shujaaz* #39, ukurasa wa 18-23), Maria Kim alipopokea habari kuwa mnuna wake Brayo alimrusha mhusika Mama Stacey kwa jiwe. Shujaa Maria Kim alitafuta maoni ya wanajamii kuhusu vijana waliokosa maadili. Tazama kielelezo cha 36:



Kielelezo cha 1, *Shujaaz* chapta #39, ukurasa wa 21

Paneli ya kwanza Maria Kim aliambiwa na mhusika wa kike:

Kijana yangu alikuwa mzuri. Lakini alijoin gang, wakaanza kutumia madawa za kulevy siku hizi hata sijui ako wapi.

Kijana (mvulana) wangu alikuwa (mwenye tabia) mzuri. Lakini alijiunga na kikundi chenye sifa mbaya na wakaanza kutumia dawa za kulevy... hata siku hizi sijui aliko.

Mhusika Maria Kim alitarajiwu kutafuta suluhu ya vijana kujiunga na matumizi ya dawa za kulevy.

Paneli ya pili, mhusika aliyeketi anamwambia Maria Kim:

Josphat alisoma mpaka class 8. Alikataa kwenda form 1 siku hizi anarandaranda tu. Mimi husikia ni mwizi.

Josphat alisoma hadi darasa la nane baadaye alikataa kujiunga na kidato cha kwanza. Siku hizi yeye hurandaranda tu. Mimi husikia ni mwizi.

Maria Kim aliambiwa nukuu hii kwa matarajio kuwa angepata suluhu dhidi ya visa vya vijana kuacha shule na kushiriki wizi.

Paneli ya tatu mhusika anayeuzwa nyanya anamwambia Maria Kim:

Natamani Jemimah angekuwa kama wewe. Yeye hulewa kila wakati! Sasa nitasaidia huyo msichana yangu aje?

Ninatamani Jemimah angekuwa (na hulka njema) kama wewe.

Yeye hulewa kila wakati! Sasa nitamsaidia msichana wangu vipi?

Paneli hii ilimsawiri Maria Kim kama shujaa ambaye angeikomboa jamii kutokana na visa vya vijana kujiunga na uraibu wa kunywa pombe.

Paneli ya nne mzee katika gari la kubeba abiria anasema:

Siku moja nikapita hii street usiku nikaona msichana yangu kumbe she sells her body! My daughter.

Siku moja nilipita barabara hii usiku nikamwona msichana wangu kumbe anauza mwili wake (kahaba) msichana wangu!

Mhusika huyu alilalama kuhusu mwanawe kuwa kahaba. Kwa matarajio kuwa Maria Kim angepata suluhu la visa vya wasichana kushiriki ukahaba.

Kwa mujibu wa Phillips & Strobl (2006), uhalifu katika kazi za vikatuni hutokea kupitia nguvu za kimabavu na matumizi ya dawa za kulevyta. Ilidhihirika kuwa vijana walikuwa na uraibu wa matumizi ya dawa za kulevyta na kunywa pombe, walikataa masomo na walishiriki ukahaba. Kwa mujibu wa Fairclough (1989), lugha inapotumika na wale wenye taaluma ya tajika, tabaka la juu na nyadhifa za kisiasa kwa kawaida hutawala mfumo wa mtagusano katika jamii. Mhusika Maria Kim alitawala mkakati wa kutafuta suluhu la vijana wanaojiunga na makundi ya uhalifu.

Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi huelezea dhana ya uwezo kama kundi la watu ambalo hudhibiti shughuli mahususi ya mawasiliano. Hadhi ya Maria Kim ya kuwa shujaa ilimpa mamlaka ya kushinikiza wahusika wengine ili kuafikia malengo yake. Wahusika katika vikatuni vya muhuja huwa na nafasi bora ya kuangazia mema dhidi ya maovu katika jamii (Kading, 2005). Hali hii iliwekwa bayana kupitia kwa mazungumzo baina ya Maria Kim na JK katika kielelezo cha 37:



Kielelezo cha 2, *Shujaaz* chapta #39, ukurasa wa 20

Maria Kim: *Ninaogopa hata Brayo ataingia life ya uhalifu.*
Ninaogopa hata Brayo atajiunga na uhalifu.

JK: *Usigive up, I'm sure tunaweza get solution. Ninajua wewe. Ninajua uta-get idea ya kuwasaidia.*

Usife moyo, ninaimani tutapata suluhu. Ninajua utapatawazo la namna ya kuwasaidia.

Mhusika JK aliamini Maria Kim angekomboa jamii kutokana na hali ya vijana kuijunga na makundi ya kiuhalifu. Baadaye Maria Kim alipigania haki za vijana katika mukutano wa hadhara ulioandaliwa na bunge la gatuvi. Hatimaye, umati wa

wanajamii uliamua kushirikiana naye. Uliungana mkono pilkapilka za kuwaepusha vijana na uhalifu. Mhusika Mama Stacey aliyeongoza umati huu katika kielelezo cha 38, anasema:



Kielelezo cha 38, *Shujaaz* chapta #39, ukurasa wa 23

Mama Stacey: *Tumefika! Tume-come ku-support hiyo idea yako.
Tunajua ni ya maana sana!*

*Tumefika! Tumekuja kuunga mkono hilo wazo lako. Tunajua ni la
manufaa sana!*

Kwa mujibu wa Dittmer (2005) adui wa shujaa katika vikatuni ni adui wa jamii. Mhusika Maria Kim ni kiongozi aliyepigania vijana dhidi ya kujiunga na makundi ya uhalifu. Kwa mujibu wa Boyd (2015), kazi za vikatuni aghalabu huwa uwanja wa mapambano ya mema dhidi ya maovu. Mhusika huyu aliwakilisha waliopinga uhalifu na kukuza umoja baina ya wanajamii waliomwunga mkono.

6.3 Wahusika Mashujaa na Vijana

Sampuli ya utafiti huu ilibainisha kuwa kuna mahusiano ya uwezo baina ya wahusika mashujaa na vijana. Wahusika mashujaa walikuwa kielelezo chema kwa hadhira lengwa. Matendo na lugha ya mashujaa katika mitagusano yao na hadhira si chombo bia cha mawasiliano. Aghalabu husheheni maslahi ya makundi yenye uwezokatika kushinikiza mipango, maslahi na ajenda fulani katika jamii (Alvi & Baseer, 2012). Mfano, paneli ifuatayo (kielelezo cha 39) mhusika Malkia aliwaelimisha vijana kuhusu namna ya kuzuia mifugo kuharibu mimea shambani:



Kielelezo cha 39, *Shujaaz* chapta #17, ukurasa wa 12

Paneli ya kwanza, Malkia alipata wazo kuhusu namna ya kuzuia mifugo kuharibu mimea. Mchoro wa taa uliyopo juu ya kichwa cha mhusika Malkia uliashiria wazo lenye manufaa ambalo limemjia akilini kwa gafla. Mhusika kutazamana na msomaji ni ishara kuwa matukio katika paneli zilizofuata ni kwa manufaa ya msomaji. Paneli ya pili, ina maneno ya mwandishi “chukua mbolea ya mbuzi” (chukua samadi ya mbuzi) weka kwenye ndoo. Paneli ya tatu, msomaji alishauriwa aunde mchanganyiko wa maji na samadi. Hatimaye, apake mchanganyiko huo kwenye majani ya mimea. Paneli zilizofuata mbuzi walipokaribia mimea iliyopakwa mchanganyiko na kujaribu kula wanashindwa.


Hatua baada ya nyingine vijana walifunzwa namna ya kuzuia mifugo kuharibu mimea. Kwa mujibu wa Nesler & Wengine (1993), imani, maarifa na maoni hupokelewa na kuaminika katika diskosi kutokana na kile wapokeaji wanachokiona kuwa na mamlaka yanayotokana na wasomi, wataalamu au vyombo vya habari vya kuaminika. Kutokana na umaarufu wa Malkia ni matarajio ya mwandishi kuwa vijana wafugaji wangeiga namna ya kuzuia mifugo kuharibu mimea kwa paneli hizi.

6.4 Wadhamini na Vijana

Uchanganuzi makinifu wa diskosi huchunguza diskosi ili kubainisha namna miundo, mikakati au vipengele vingine vya usemi, mazungumzo au matukio ya mawasiliano yanavyojukumika katika uzalishaji wa mahusiano yasiyokuwa na usawa (Fairclough & Wodak, 1997). Wadhamini huwa na uwezo wa kiuchumi kuliko vijana. Hali hii iliwapa wadhamini mamlaka ya kudhibiti na kushinikiza matendo ya vijana. Uwezo huu ultokana na wao kuwa na rasilimali iliyowawezesha kudhibiti uwasilishaji wa maslahi yao katika diskosi ya *Shujaaz* (Van Dijk, 2008).

Van Dijk (2008), anadai kuwa uchanganuzi makinifu wa diskosi hutumiwa kutathmini maana ya umaanisho kuhusu ubaguzi wa rangi, nafasi ya kitabaka na hegemoni. Kwa mujibu wa Fairclough (1995), hegemoni ni namna mamlaka ya kundi tawala yanavyokubaliwa na kuhalalishwa kupitia kwa sheria, tambiko za jamii, mawasiliano na hulka. Wasomi wa uchanganuzi makinifu wa diskosi huitazama hegemoni kuwa njia ambayo fikira na matendo hukubaliwa katika jamii (Fairclough, 1989). Hegemoni ya wafadhili katika diskosi ya *Shujaaz* ilitamalaki kwa sababu ya vijana kukosa uwezo wa kuamua kinachochapishwa. Uwezo ambao huenda wadhamini wanao. Aidha, vijana huenda walikosa maarifa na imani iliyohitajika kupinga diskosi au maslahi ya wadhamini (Wodak, 1987).

Uchanganuzi makinifu wa diskosi ni uchanganuzi wa miktadha mbalimbali ya mitagusano ya jamii kwa minajili ya kuweka wazi namna matumizi ya lugha husheheni itikadi na mahusiano ya uwezo (Fairclough & Wodak, 1997). Jarida la *Shujaaz* ni jukwaa ambalo wadhamini hutangaza bidhaa, huduma na kueneza itikadi yao. Itikadi hii hupata mamlaka na uhalali wake kutokana na kibali cha hiari wala si kwa nguvu. Kwa mujibu wa Eagleton (1991), itikadi ni maslahi ya kundi mahususi la watu na hurejelea mawazo na imani inayoashiria hali na tajriba ya kundi mashuhuri au tabaka la juu. Vijana hawana budi ila kusoma hadithi iliyosheheni maslahi ya wadhamini. Kielelezo cha 40 kina michoro ya majumba yaliyo na nembo ya kampuni ya *Safaricom*:



Kielelezo cha 40, *Shujaaz* chapta #39, ukurasa wa 3

Panelini nembo ya kampuni ya *Safaricom* iko kwenye michoro ya majumba. Imani iliyorithishwa na tangazo hili ni kuwa kampuni ya *Safaricom* ilihuushwa na umati wa watu. Majumba yalikaribiana na mukutano wa baraza la chifu ambalo huenda lingehudhuriwa na umati wa watu. Tangazo hili liliazimia kuwashawishi vijana kukubali umaarufu wa huduma za *Safaricom*.

Kwa mujibu wa Raskin (2008), vikatuni hutumika kufficha hisia halisi na imani “kwa sababu huficha kile ambacho hakiwezi kusemwa hadharani.” Vikatuni vinavyorejelea kinachosemwa kwa uwazi, hukosa mashiko na havitekelezi wajibu uliokusudiwa. Nembo hii ilitangaza na kuhalalisha maslahi ya kampuni ya *Safaricom* dhidi ya maslahi ya kumpuni pinzani (Eagleton, 1991). Japo si kwa njia ya moja kwa moja. Wanavyosema Ivan & Clark (1997), ni kuwa watu hawapati maana katika ombwe tupu. Matumizi ya lugha husheheni muktadha wa kijamii. Muktadha wa kimazingirani panelini nchini Kenya. Lengo la kuwepo kwa nembo ya kampuni ya *Safaricom* katika diskosi ya *Shujaaz* ni fiche. Illichanganuliwa kimakinifu ili kufichua maslahi yaliyoendelezwa na nembo hii.


Lengo la nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi ni kubainisha mwingiliano na mahusiano yaliyofiche ili yasioneokane na watu (Fairclough, 1995). Nadharia hii inajihuisha na mahusiano baina ya matumizi ya diskosi na uwezo. Kuwepo kwa istilahi *Safaricom* ni njia moja ya kujenga hegemoni katika soko la huduma za

mawasiliano. Kwa mujibu wa Van Dijk (1993), nguvu na shinikizo kutoka kwa wenyewe uwezo hujumuishwa katika sheria na miiko na huchukua mfumo wa hegemoni. Nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi hutazamia kubainisha mahusiano ya uwezo na huweka wazi majukumu ya diskosi katika kuzalisha au kupinga matumizi mabaya ya mamlaka. Nembo hii iliwashinikiza vijana kwa njia ambao si wazi kutumia huduma za kampuni ya *Safaricom* badala ya kampuni pinzani.

6.5 Hadhira na Mtu Mashuhuri

Mtu mashuhuri katika *Shujaaz* huangaziwa chini ya anwani *Celeb*. Huwa kijana mwenye wafuasi wengi ambao ni vijana na amepitia maisha yenyе changamoto na baadaye akafaulu. Aidha, ni bingwa katika uimbaji, upigaji picha, uigizaji na uchekeshaji. Hueneza masuala fulani yenyе chembechembe za imani za kiiikadi katika *Shujaaz*. Kwa mujibu Sturken & Carwright (2001), kiiikadi, vikatuni ni njia ambayo itikadi huzaliwa na kusawiriwa katika jamii vinamosomwa. Huangazia mitazamo ya kisiasa, kuhimiza itikadi na kuendeleza mahusiano ya uwezo katika jamii (Lewis & Wengine, 2008). Muundo wa lugha katika diskosi ya *Shujaaz* ulikuza mwonoulimwengu na mitazamo mahususi kuhusu aushi ya mtu mashuhuri (Barrat, 1994).

Mfano, katika *Shujaaz* chapta #82, ukurasa 8, umaarufu wa mwanamuziki Khaligraph Jones ulimpa hadhi kubwa katika jamii kuliko vijana. Ilisababisha apewe fursa ya kusimulia tajriba ya maisha yake kupitia kwa mahojiano. Huenda vijana wangeiga mkondo wa maisha uliohimizwa na mtu mashuhuri. Mfano wa paneli zilizoangazia mahojiano baina ya DJ Boyie na Khaligraph Jones ni kielelezo cha 41:



Kielelezo cha 41, *Shujaaz* chapta #82, ukurasa 8

Khaligraph Jones, alihoji kuwa alizaliwa katika mtaa wa mabanda wa 1961 Kayole viungani mwa jiji la Nairobi. Mahusiano ya uwezo baina ya mwanamuziki huyu na vijana ni wa aina mbili; kwanza anahadhi kuliko vijana kwa sababu ya umaarufu wa kuwa na kipaji cha uimbaji. Anavyosema Scotton (1993), ni kuwa lugha huonyesha hadhi ya wazungumzaji katika mazingira tofauti na wao hubadili msimbo ili kukidhi mahitaji ya muktadha wa mazungumzo. Aidha, lugha ni kigezo cha kupima mamlaka waliyo nayo watu. Hatimaye, mwimbaji Jones, alitumia mahojiano haya kujiweka katika kiwango kimoja cha uwezo na vijana waliozaliwa katika mitaa ya mabanda kama yeche.

Alikuza uhalisia wa mazungumzo kwa kutaja mtaa wa mabanda ambao upo katika ulimwengu wa uhalisi. Alitumia hadhi ya kuwa *Celeb* katika jamii kuwashauri vijana kuhusu mada mbalimbali. Tazama kielelezo cha 42:



Kielelezo cha 42, *Shujaaz* chapta #82, ukurasa 9

DJ Boyie: *Unaweza show mafans ujanja gani iki-come mambo na Bizz*
Unaweza washauri vipi mashabiki kuhusu masuala ya
(kuanzisha) biashara.

